# Nipashe

Jumanne Oktoba 13, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580367

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





**MDEE** kufunguka madai zuio kampeni

UKURASA 3



**KAMPUNI** kuchapisha karatasi kura yatajwa

UKURASA 5

**Rais akataa Messi ni mbeleko ya LaLiga**

UKURASA 22

# JPM asema Tanzania ina maadui wengi nje

• **Ataja** hujuma katika miradi, rasilimali, aagiza maeneo matatu ya kupatiwa maji Dar... *Endelea uk.2*



Mgombea urais kupitia CCM, Dk. John Magufuli akiwasalimia wanachama wa CCM, baada ya mkutano wa kampeni uliofanyika Kinyerezi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 7
**70% MOTO MLIMA KILIMANJARO WADHIBITIWA**

UKURASA WA 9
**MKURUGENZI AKERWA WATOTO KUOGESHWA DAWA ZA MAPENZI**


## Lissu azidi kuchanja mbuga mikoa ya kati

UKURASA 3



Mgombea urais kupitia CHADEMA, Tundu Lissu, akiwasili mjini Nzega mkoani Tabora jana, kwa ajili ya mkutano wa kampeni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Benki Kuu yaongezea VICOBA miezi sita

UKURASA 5




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein (katikati), akiwa na mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi na mke wa mgombea huyo, Mama Mariam Mwinyi, wakifungua pazia kuashiria ufunguzi wa nyumba za maendeleo Mji Mpya wa Kwahani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# JPM: Tanzania ina maadui wengi

**Na Gwamaka Alipipi**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amesema hatua alizozichukua ikiwamo kudhibiti utoroshaji wa madini, ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme, kuushinda ugonjwa wa virusi vya corona, kumesababisha Tanzania kujitengenezea maadui wengi ndani na nje ya nchi.

Amesema baadhi ya mataifa hayo ya kigeni adui wao namba moja ni yeye (Rais Magufuli), kulikosababishwa na kuwazibia mianya ya ulaji wakati wa utawala wake.

Aliyasema hayo jana kwenye kampeni za uchaguzi mkuu, wakati akiomba kura kwa wakazi wa Wilaya ya Ilala eneo la Kinyerezi, mkutano uliohudhuriwa na maelfu ya wananchi pamoja na wanachama wa CCM.

"Ndugu zangu tumejitengenezea maadui. Hatua tunazozichukua haziwafurahishi. Ujenzi wa ukuta Mirerani, usitishwaji wa usafirishaji wa makinikia, ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere, kuishinda corona, hawawezi kufurahi, lazima watuchukie kwa sababu walitaka kuigeuza Tanzania sehemu ya kuchuma," alisema Dk. Magufuli.

**MADINI TANZANITE**

Dk. Magufuli alisema awali madini ya Tanzanite yalikuwa yanasombwa usiku na mchana na kusafirishwa kwenda nje ya nchi, huku Tanzania ikibakiwa na mshimo na kutoambulia chochote.

Alisema Tanzania haikuwa katika nafasi ya kwanza wala ya pili wala ya tatu kwa uuzaji wa madini ya Tanzanite duniani, licha ya madini hayo kupatikana pekee nchini.

"Nilipoingia madarakani nikaanza kujenga ukuta eneo lote la uchimbaji, watu wakaanza kunishangaa, lakini leo faida tunapata, tumefunga 'camera' tuna monitor' (uangalizi) na akina Laizer leo wamepatikana. Hao watu hawawezi kufurahi lazima watuchukie sisi".

Kuhusu madini ya dhahabu, Dk. Magufuli alisema mataifa ya kigeni yalikuwa yanachimba madini hayo na kuyasafirisha kwao kwa kisingizio cha kusafirisha mchanga. Alisema mikataba ya uchimbaji madini ilikuwa inasainiwa nje ya nchi.

Alisema alipoingia madarakani alipiga marufuku usafirishaji wa makinikia, mikataba ya uchimbaji ikiaanza kusainiwa hapa nchini.

"Eti wanachukua mchanga na kuusafirisha kwenda kwao, kama ulikuwa ni mchanga kwa nini wasiuache hapa hapa au wakautumia kwenye ujenzi? Tukawabana, tukaanzisha kampuni ya Twiga na wakaleta faida ya Sh. bilioni 100 na zingine wanaleta hivi karibuni. Kwa hiyo adui yao namba moja ni mimi kwa sababu nakwamisha mambo yao," alisema Dk. Magufuli.

**UGONJWA WA CORONA**

Dk. Magufuli alisema wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, mataifa ya Ulaya yalitoa maagizo kwamba, ili kuushinda ugonjwa huo ni lazima serikali iwafungie ndani wananchi wake na kuvaa barakoa muda wote.

"Kati ya kipindi kigumu nilichopata ni kile... nikaanza kumuomba Mungu, tukaanza uchunguzi kwa kuyapima mapapai na tukayakuta na corona. Nikasema huu ni mchezo mchafu. Walitaka kutuletea chanjo, kutuuzia dawa, ili wapate pesa. Niliwakwamisha. Nikasema tutamwomba Mungu corona itaondoka, leo haipo. Na sasa wanatumia mbinu za kila aina ikiwamo kuleta wasaliti, wanatuma watu watutukane, lakini Tanzania bado tupo imara."

**BWAWA LA MWALIMU NYERERE**

Dk. Magufuli alisema uamuzi wa serikali kujenga bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere, kumeyachukiza mataifa ya Ulaya kwa sababu walikuwa wana miradi yao, iliyokuwa inawaingizia pesa kwenye mbuga ya Selous.

Alisema walikuwa na vitaru 41 vya uwindaji pamoja na viwanja vidogo vya ndege 32, ambavyo walikuwa wanavitumia kusafirishia meno ya tembo na nyara zingine za serikali.

Alisema hata serikali ilipoanza utafiti wa kuanza kujenga, mataifa hayo yaliweka masharti, ambayo yalikuwa yanakwamisha kuanza kwa ujenzi.

"Kwa hiyo ndugu zangu Watanzania, hawa watu hawawezi kutupenda, walikuwa wanatuchezea sana, tumeibiwa mno, tumetengeneza maadui wengi," alisema Dk. Magufuli.

**AHAKIKISHIA VIJANA AJIRA**

Wakati huohuo, Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo atawajali vijana kwa kuwahakikishia ajira za uhakika.

"Nitawajali vijana, ndani ya miaka mitano ijayo nitashughulikia tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Kama tumejenga flyover nitashindwaje kuwatengenezea ajira vijana. Mniamini," alisema Dk. Magufuli.

Pia, aliwahakikishia kinamama, wazee wanaonyanyaswa na kuteseka kuwasaidia kuondokana na mateso yao.

"Tumepanga kuwatumikia wana Dar es Salaam bila ya ubaguzi, mimi huwa naumia sana ninapoona wazee, kinamama wanaponyanyaswa na kuteseka".

## ...Aagiza maeneo matatu kupatiwa maji Desemba

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amemwagiza Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, kuhakikisha maeneo ya Kinyerezi, Bonyokwa na Kifuru, jijini Dar es Salaam yanapata huduma ya majisafi na salama ifikapo Desemba, mwaka huu.

Alitoa agizo hilo jana wakati akiwa katika mkutano wa kampeni kwenye kata ya Kinyerezi wilayani Ilala, alipokuwa akizungumza na wananchi wa maeneo hayo, pamoja na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Kama kuna Waziri wa Maji ananisikia basi anisikie vizuri, hii ni amri ya John Pombe Joseph Magufuli, hayo maeneo ya Kinyerezi, Bonyokwa na Kifuru, waanze kunywa majisafi na salama ifikapo Desemba, mwaka huu," alisema.

**AELEZA CHANGAMOTO**

Aidha, alieleza changamoto alizokutana nazo wakati akiingia madarakani mwaka 2015, mojawapo ikiwa ni kuhakikisha vitendo vya ujambazi vinatokomea katika Jiji la Dar es Salaam.

"Niliupata urais bila ya kutumwa na mtu, wala kuhonga. Nilipoingia madarakani nilikutana na changamoto ikiwamo baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam kutokuwa na amani, polisi waliuawa Kibiti, mkoani Kigoma watu walikuwa wanatekwa, wanauawa, Ubungo mchana majambazi walivamia benki na kupora fedha. Nikasema nitakomesha," alisema Rais Magufuli.

Alisema Jiji la Dar es Salaam lilikuwa limekithiri matukio ya ujambazi, wafanyabiashara wa maduka walikuwa wanavamiwa na kuporwa mali zao mchana.

"Yaani jambazi alikuwa anakupigia simu anakuambia leo nakuja kuchukua pesa na kweli anakuja na kupora. Nikasema jambo la kwanza ni kujenga amani ya Watanzania, na hili tumelifanya vizuri japokuwa bado kuna changamoto," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema kila kitu katika Jiji la Dar es Salam kilikuwa ni shida, ikiwamo wajasiriamali kuteseka na kwamba alianza kujenga 'fly over' pamoja na barabara.

"Wajasiriamali waliteseka, kila sehemu walikuwa wanafukuzwa, ndiyo maana nikaamua kuwatengenezea vitambulisho kwa gharama ya Sh. 20,000 kwa mwaka, awali walikuwa wanalipa Sh. 1,000 kwa siku. Leo wanafanya biashara kwa uhuru, hawabugudhiwi," alisema.

Alifafanua kuwa dhamira ya serikali ni kuona Watanzania wanakuwa na maisha mazuri kwa kupata huduma bora za kijamii, ikiwamo kushusha bei ya umeme miaka ijayo.

"Ninataka bei ya umeme ishuke iwe kama kwao (Ulaya). Ila nawashangaa baadhi ya Watanzania wanazunguka Ulaya wanasema Tanzania inyimwe mikopo, wanatutukana. Nawaomba Watanzania muwapuuze."

Aliwataka wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kumpigia kura nyingi ili awe Rais kwa awamu ya pili na kwenda kutekeleza mambo ambayo bado hajayatimiza.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge, wakikagua uchimbaji wa kisima kinachojengwa eneo la Ihumwa, jijini Dodoma jana. **PICHA: HAPPINESS SHAYO**

## Mdee kufunguka madai kusimamishwa kampeni

**Frank Maxmillian (TUDARCo) na Evelineema Ernest (SJMC)**

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Kawe, kwa tiketi cha Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Halima Mdee, amesema kuwa leo atafunguka yote kuhusu tetesi za kufungiwa kwake.

Juzi katika ukurasa wake wa Tweet aliandika kuwa amezuiliwa kufanya kampeni kwa siku saba kwa kile kilichoelezwa ni kukiuka maadili, na baadaye taarifa hizo kusambaa kwenye mitandao ya kijamii.

"Ni kweli nimezuiwa kuendelea na kampeni kwa siku saba, ila kesho (leo) nitazungumza na waandishi wa habari kufafanua kila kitu,"aliliambia Nipashe kwa njia ya simu. Juzi, katika ukurasa wake aliandika: "Nimepata taarifa nimefungiwa kufanya kampeni siku saba kuanzia Oktoba 12 hadi 18, mwaka huu...tutaweka wazi ushahidi tuliowasilisha kikao cha maadili."

Nipashe ilimtafuta Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Kawe, ambaye simu yake ya mkononi ambayo iliita bila kupokelewa na hata alipotumiwa ujumbe mfupi haukujibiwa.

## TLP yasema inaendelea kumuunga mkono JPM

**Na Richard Makore,** MWANZA

CHAMA cha Tanzania Labor Party (TLP), kimeibuka na kusema kuwa bado kina nia ya kumuunga mkono mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), John Magufuli (pichani) katika uchaguzi mkuu ujao.

Kimesema Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini Tanzania ilikosea kutangaza kwamba wamesitisha uamuzi huo.

Akizungumza na Nipashe, Makamu Mwenyekiti wa TLP, Domina Rwechngura, alisema msimamo wao upo pale pale wa kuendelea kumuunga mkono mgombea huyo.



"Sisi tuliishasema tangu mwezi wa tano kwamba tutamuunga mkono Rais Magufuli katika uchaguzi huu, hivyo msajili kauli yake kwamba tumesitisha uamuzi wetu hatuitambui," alisema.

Hivi karibuni vyama vya TLP na UDP viliripotiwa kujiondoa mpango wa kumuunga mkono mgombea urais wa CCM, kutokana na kutofuata kanuni na sheria za uchaguzi.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, hivi karibuni alisema waliwaambia TLP na UDP suala hilo lina utaratibu ambao walitakiwa kuufuata, na walipoona hawajafuata, vyama hivyo vimekaa kimya na havisikiki tena.

Aliongeza kuwa UDP waliendelea na kazi zao za kampeni, wakiwa na mgombea wao na kutangaza sera za chama chao.

Vile vile, alisema TLP ambao waliweka mabango wameyatoa na wanaendelea na kampeni zao.

# Tundu Lissu ajinadi mikoa 3

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ameendelea kuchanja mbuga kwenye mikoa ya Singida, Tabora na Shinyanga huku akisema uchaguzi huu hautakuwa rahisi kwa kuwa kura ya mwaka huu ni ya ukombozi wa nchi.

Akizungumza jana katika mikutano tofauti ya maeneo ya Iramba mkoani Singida, Igunga na Nzega Mjini mkoani Tabora na Kagongwa wilayani Kahama, alisema kuwa Watanzania wajitokeze kwa wingi kupiga kura na kumpa ushindi ikiwamo kulinda kura.

Alisema kwa miaka mitano baadhi ya wananchi wamepitia changamoto mbalimbali ikiwamo ya watu kujeruhiwa, kupoteza maisha, kujeruhiwa na wengine kuwa na kesi katika Mahakama mbalimbali nchini.

Alisema kura ya mwaka huu ni muhimu sana kwa kuwa ndiyo wakati wa ukombozi kwa Watanzania kuondokana na madhila mbalimbali, huku akitaja baadhi ya matukio ikiwamo la yeye kushambuliwa kwa risasi mwaka 2017.

"Chagueni mtu wa haki na atakayesimamia haki kwa maneno na vitendo na kwa maendeleo ya watu, ifikapo Oktoba 28, mkapige kura ili Oktoba 29, tuondokane na kero ya vitambulisho vya machinga," alisema, huku akimtaka mmoja wa wananchi aliyenyanyua kitambulisho kujibu maswali.

"Naomba uwambie wananchi wa Nzega kama hicho kitambulisho kina jina lako, waambie kama kina picha yako, waambie kama kimeeleza unapokaa au unapotokea, kama kina mwaka wa kuzaliwa na sahihi yako, umekinunua 20,000?" Alihoji.

Kwa mujibu wa Lissu, anataka kujenga nchi ya watu walio huru kukosoa na kuzungumza mawazo yao, na kutaka wananchi wanaochukizwa na hayo kupigakura kwa wingi.

"Tunahitaji kura hata ya CCM, kwa sababu tunahitaji kura ya kila mmoja, kama mtu anasikiliza mkutano na ni CCM mwacheni sababu tunahitaji kura zao," alisema Lissu.

Alisema kura ya wananchi hao kwa chama hicho, Igunga, itawaondolea kero wanayoipata kutoka kwa Mmalaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya kodi kubwa zinazowaumiza.

"Kwa mwaka huu uchaguzi hautakuwa rahisi, namna pekee ya kushinda ni kupiga kura, nchi nzima iimbe. Tukapige kura kwa ajili yetu, watoto wetu, wajukuu wetu sababu ni kura ya ukombozi, iwe kura ambayo itainua haki na haitatapanya mali," alisema Lissu.

Aidha, Lissu alisema wasimamizi uchaguzi kwenye maeneo ya kupigia kura iwapo watakataa kuwaapisha mawakala wao, itakuwa ni kinyume cha kanuni za taratibu za uchaguzi.

"Mawakala kuingia kwenye vituo vya kupigia kura baada ya majina kuwasilishwa, msimamizi wa uchaguzi ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri akipewa majina ni haki yao kuwapo hapo," alisema.

Alisema askari Polisi watakaofuata kanuni na sheria hawapaswi kuwa na hofu katika utekelezaji wa majukumu yao, na kwamba serikali ya CHADEMA itawalinda ikiwamo kujali maslahi yao ambayo alidai hayajaboreshwa kwa miaka mitano.

Aidha, alilaani uamuzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuwaengua wagombea wa CHADEMA kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kuzuiliwa kufanya kampeni na matukio ya kupigwa na kuuawa kwa baadhi ya wafuasi wa chama hicho bila hatua kuchukuliwa kwa haraka.

bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA**. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
| --- | --- | --- |
| 1 | A BETTER LIFE INVESTMENT/ PAYAS REUBEN MOREMI | Nyumba ya makazi yenye hati na.51480 PLOT na668/1 NA 690/1 BLOCK E GONGO LA MBOTO AREA. Dar es salaam kwa jina la **PAYAS REUBEN MOREMI** |

MASHART YA MNADA

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

21594032

**MAWASILIANO:**

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Bank of Africa
Head Office,
NDC Development House, ohio street-kivukoni
P.O. BOX 3054,
DAR ES SALAAM
Tel: +255-22-2110104/2111290
Fax: +255-22-2113740

bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANC ABC** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
| --- | --- | --- |
| 1 | CHRISTOPHER BERNARD MAKOMBE | Nyumba iliopo kwenye kiwanja nyumba ambayo haijakamilika iliyopo kwenye kiwanja chenye hati na .13435 kiwanja na 53, kitalu B part ii, Tabata manispaa ya ilala Dar es salaam kwa jina la **CHRISTOPHER BERNARD MAKOMBE.** |

MASHART YA MNADA

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

21594022

**MAWASILIANO:**

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Bank of Africa
Head Office,
NDC Development House, ohio street-kivukoni
P.O. BOX 3054,
DAR ES SALAAM
Tel: +255-22-2110104/2111290
Fax: +255-22-2113740

# Ulaji nyama, samaki duni

**Na Christina Mwakangale**

LICHA ya ongezeko la uzalishaji wa samaki, nyama na maziwa ikiwamo mazingira bora ya uwekezaji sekta ya uvuvi na mifugo, ulaji wa bidhaa hizo, ni duni kwa Watanzania.

Uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kufikia tani 701,679.1 mwaka 2019/2020, kutoka tani 690,629 mwaka 2018/2019 huku maziwa ikiwa, samaki tani 417,936 mwaka 2016 hadi tani 816,964 mwaka 2020.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, aliyasema hayo kwenye maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani kitaifa iliyofanyika mkoani Njombe, Oktoba 10, mwaka huu. Alisema kwamba, pamoja na ongezeko hilo, bado ulaji wa nyama na maziwa nchini sio wa kuridhisha na kutoa rai kwa wananchi kuongeza ulaji wa bidhaa hizo za chakula.

"Ili tuweze kufikia kiwango cha Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO) cha kilo hamsini za nyama kwa mwaka kwa mtu mmoja na unywaji wa maziwa kufikia lita 200, inabidi tuongeze ulaji," alisema Dk. Tamatamah.

Alisema kuwa Tanzania na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN), huadhimisha siku hiyo kila mwaka, lengo likiwa ni kukumbushana wajibu wa kila mmoja kuzalisha, kuhifadhi chakula salama ili kukabiliana na janga la njaa, kuanzia ngazi ya kaya na taifa.

"Maadhimisho ya mwaka huu yamebeba kaulimbiu inayosema 'Kesho njema inajengwa na Lishe Bora Endelevu. Hii inatutaka kila mmoja kujua kwamba suala la lishe bora ni muhimu kwa afya zetu hasa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na wazee," alisema katibu mkuu.

Alieleza kwamba, Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika sekta za mifugo na uvuvi, ndizo sekta mama katika uzalishaji wa mazao yenye viwango vikubwa vya protini nchini. Dk. Tamatamah uvuvi unachangia asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama na kutoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5 katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na sekta hiyo.

Alibainisha kuwa mwaka 2019/20, sekta ya uvuvi ilikua kwa kiwango cha asilimia 1.5 na kuchangia Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia 1.71 na pia uzalishaji wa samaki kutoka maji ya asili kwa mwaka 2019/20 umekua kufikia takribani tani 497,567 na katika uzalishaji wa mazao ya viumbe maji kufikia tani 18,716.56.

"Hata hivyo wastani wa ulaji wa samaki kwa mtu kwa mwaka hapa nchini umeongezeka kutoka kilo 8.2 mwaka 2018/2019 hadi kufikia kilo 8.5 mwaka 2019/2020, licha ya FAO kuwa na kiwango cha ulaji samaki duniani kiwe ni kilo 20.3 kwa mtu kwa mwaka," alieleza katibu mkuu.

Pia uzalishaji wa mayai uliongezeka nchini kutoka mayai bilioni 3.58 mwaka 2018/2019 hadi bilioni 4.05 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Pamoja na ongezeko hili, nawasihi wafugaji na wakulima kuendelea kujifunza teknolojia mbalimbali zinazooneshwa hapa uwanjani.



Mwonekano wa ujenzi unaoendelea wa daraja jipya la Tanzanite, lenye urefu wa km 6.3, litakalounganisha maeneo ya Aga Khan Upanga Mashariki na Ufukwe wa Coco Oysterbay kupitia Bahari ya Hindi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mgambo wapewa jukumu udhibiti wahamiaji haramu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Deodatus Kinawilo, amewataka vijana wanaopatiwa mafunzo ya mgambo, kuwa walinzi wa mipaka ya nchi na kutoruhusu wahamiaji haramu kuingia.

Akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya mgambo kwa vijana 132 wa Kata ya Nyakibimbili, Kinawilo alisema Mkoa wa Kagera unapakana na nchi za Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya, hivyo unahitaji vijana makini na wazalendo katika kulinda usalama wa nchi.

"Mkoa uko mpakani na tuna tatizo la wahamiaji haramu, lakini bado nchi iko salama na lazima nchi yetu ilindwe kwa namna yoyote ile, kwa hiyo sitarajii mtu afundishwe hapa badala ya kuwa mfano wa kuigwa, aende kufanya fujo mtaani," alisema Kinawilo.

Alisema mafunzo hayo yapo kwa mujibu wa sheria inayotaka kila kata kuwaandaa vijana wa kulinda wananchi na mali zao, na kwamba ndiyo maana Tanzania iko salama kwa sababu ya uwapo wao.

Baadhi ya vijana wanaopatiwa mafunzo hayo Ghati Thomas na Benetson Wilbard wamewataka vijana wanaohitimu mafunzo hayo kuzingatia maadili na kuepuka kujihusisha na vitendo vya kihalifu, huku wakiiomba serikali kuwasaidia kupata kazi katika kampuni za ulinzi na maeneo mengine yanayojitaji ulinzi.

"Hatua kali zichukuliwe kwa vijana watakaobainika kujihusisha na uhalifu, ili jeshi letu liendelee kuheshimiwa na watu wote, maana anayepatiwa mafunzo haya anapaswa kulinda nchi na sio kwa kushiriki vitendo visivyofaa," alisema Ghati.

Akisoma risala kwa mkuu wa wilaya hiyo, mmoja wa washiriki, Bashiru Mussa, wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kutishwa na baadhi ya wananchi kutokana na uelewa mdogo wa jamii juu ya mafunzo hayo, na baadhi ya vijana kukimbia mafunzo.


**KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA**

**EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA**

**Ref No: elcthq/2020/HD/350**

**Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, kupitia idara ya afya inatangaza Zabuni ya ununuzi wa vifaa Kinga kwa ajili ya vituo vya Huduma afya**

**Masharti ya waombaji;**

1. Awe Anafanya Biashara katika mkoa wa Arusha
2. Awe na uzoefu wa usambazaji wa vifaa kinga kwa idadi inayohitajika
3. Awe amesajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania na ni mlipa kodi

| S/N | Aina ya Vifaa | Maelezo | Idadi |
|---|---|---|---|
| | Mask Surgical, | type IIR, Disposable | 6,000 |
| | Mask | high-fil FFP2/N-95 NO-Valve | 500 |
| | Gown Surgical | Non-woven Disposable | 1,440 |
| | Apron, Protection | Plastic, Reusable | 240 |
| | Boots Rubber, | PVC, Reusable | 240 |
| | Glasses, Safety | Regular size | 240 |
| | Gloves Examination , | Non-sterile (50 pair perbox) | 360 |
| | Utility Gloves, | Heavy Duty, Rubber | 480 |
| | Ethanol (5 liters) | 70% Alcohol | 720 |
| | Hydrohen Peroxide | Strength 5% | 480 |
| | Glycerine | Dozen botles of 100mls each | 240 |

**Maombi yote yatumwe kwa**
**Katibu Mkuu**
**KKKT Makao Makuu**
**S.L.P 3033 Arusha . Simu 0767 666 165/0767 955 069**

Bahasha iliyofungwa kwa Lakiri iandikwe juu **"UNUNUZI WA VIFAA KINGA'.**
Nyuma indikwe **jina, anwani ya mwombaji na namba za simu.**
Mwisho wa kupokea maomni ni 19/10/2020 siku ya Jumatatu saa kumi kamili Jioni


# ATE: Waajiri wapeni mafunzo wahitimu

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), kimewakumbusha waajiri kutoa programu za mafunzo mahala pa kazi kwa wahitimu, ili kutengeneza fursa za ajira, ambazo zitawezesha kuajirika na kuendana na kasi ya sasa ya nchi kufikia uchumi wa kati.

Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa chama hicho, Dk. Aggrey Mlimuka, alitoa wito huo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza kuhusu kampeni ya kuhamasisha programu ya uanagenzi na mafunzo mahali pa kazi pamoja na uzinduzi wa wiki ya huduma kwa wanachama iliyoanza siku hiyo.

Alisema ATE kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) wamezindua kampeni yenye lengo la kuongeza uelewa miongoni mwa waajiri Tanzania kuhusiana na umuhimu wa uanagenzi na programu nyingine mahala pa kazi kwa wahitimu, ili kutengeneza fursa za ajira na kusababisha vijana wawe na sifa za kuajirika.

"Kama mnavyofahamu hivi karibuni Tanzania ilifanikiwa kuingia katika nchi zenye kipato cha uchumi wa kati, huku suala la kuendeleza ujuzi likiendelea kuwa kiungo muhimu katika kufikia hatua hii kubwa kiuchumi," alisema.

Pia alisema suala la kuendeleza ujuzi ni kipaumbele kilichopo katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, ambapo serikali imeshakamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wake na sasa ni awamu ya pili inayosisitiza watu wenye ujuzi wa kutosha.

Mlimuka alisema miongoni mwa faida kwa mwajiri anazozipata pindi anapotoa mafunzo ni pamoja na kutengeneza wafanyakazi wenye ujuzi katika nadharia katika kampuni husika.

Pia alisema hutengeneza wafanyakazi wanaoifahamu vizuri kampuni na kuwafanya wakae muda mrefu.

"Hupunguza gharama za uendeshaji kwa kampuni kwa sababu mfanyakazi atakuwa anajifunza huku akifanya kazi na kupewa posho kidogo kwa ajili ya kujikimu," alisema.

Mlimuka alisema programu za mafunzo huwasaidia vijana wengi kuwa na ujuzi unaowafanya waajiriwe. Kuhusu wiki ya huduma kwa wanachama, Mlimuka alisema ATE inawapatia fursa wanachama wake watoe mrejesho kuhusiana na huduma za chama.

"Tuna kliniki ya huduma ya msaada wa sheria za kazi na ajira kwa wanachama na wasio wanachama, ili waweze kuuliza maswali kwa Mwanasheria wa ATE, pia tunapokea mrejesho wao, mapendekezo na ushauri, tunawakaribisha," alisema.

Alisema ATE kilianzishwa mwaka 1960 na kusajiliwa chini ya sheria ya ajira na mahusino kazini Novemba 14, mwaka 2007 na kwa sasa kina wanachama zaidi ya 1,500 wa moja kwa moja na zaidi ya 1,700 waliochini ya mwamvuli wa vyama vya kisekta.

## HABARI KITAIFA



Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Rhoben Nkori (wa pili kulia), akikabidhi cheti kwa mmoja wa makandarasi walioshiriki mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na bodi hiyo mkoani Arusha. Kulia ni Naibu Msajili wa bodi hiyo, David Jere, (wa nne kulia) ni Mratibu wa Mafunzo wa bodi hiyo, Neema Fuime na Meneja wa CRDB Kanda ya Kaskazini, Sauda Njila. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# VICOBA vyaongezewa miezi sita usajili leseni

**Na Christina Mwakangale**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imeongeza miezi sita kwa ajili ya maombi ya leseni na usajili kwa watoa huduma za fedha ikiwamo Vikundi vya Kifedha vya Kijamii (VICOBA).

Kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa mwaka jana mwisho wa usajili ulitakiwa kuwa Oktoba 31, mwaka huu, na kwa mabadiliko hayo ni hadi Aprili 30, mwaka 2021.

Hivi karibuni iliibuka taharuki kwenye vikundi mbalimbali vingi vya wanawe ambao huweka fedha kwa lengo ya kukopeshana na kusaidiana kwa shida na raha za kijamii, kukosa mwongozo wa namna ya kupata leseni husika zaidi ya kusajili ngazi ya halmashauri na manispaa.

Hali hiyo, pia ilikuwa kwa kampuni binafsi zinazopokea amana na kutoa mikopo kufuatia agizo la BoT kuagiza wajisajili, kabla ya Oktoba 31, mwaka huu.

Agizo hilo liliwahusu watoa huduma za fedha walio katika daraja la kwanza hadi la nne ikiwamo, benki, taasisi, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), VICOBA, Upatu.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, jana, uamuzi huo ulitokana na maombi ya wadau wengi kuomba kuwaongezea muda wa usajili na leseni, ili wawasilishe maombi yanayoendana na matakwa ya sheria na kanuni husika.

"Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kuutaarifu umma kuwa tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi ya usajili au ya leseni imesogezwa hadi tarehe 30 Aprili 2021.

Matarajio ni kwamba muda ulioongezwa utawawezesha watoa huduma ndogo za fedha katika madaraja yote kufanya maandalizi ya kutosha na kuwasilisha maombi yaliyokamilika na yanayokidhi matakwa ya Sheria na Kanuni," alisema Prof. Luoga.

Alisema ilielekezwa awali, maombi ya usajili au leseni yawasilishwe katika muda wa nyongeza uliotolewa kwa watoa huduma ndogo za kifedha walio katika daraja la pili wawasilishe maombi yao ya leseni BoT, Makao Makuu au matawi ya benki ikiwamo Arusha, Mwanza, Zanzibar, Mbeya, Mtwara na Dodoma.

Kadhalika, alisema agizo liliwataka watoa huduma hao waliopo daraja la tatu, wawasilishe maombi ya leseni katika Ofisi ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa, kupitia mfumo wa kuomba leseni wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, vilevile daraja la nne kuwasilisha maombi ya kuandikishwa katika Ofisi za Serikali ya Mitaa zilizo karibu nao.

"Benki Kuu inapenda kuutahadharisha umma kuhusu matangazo na maelekezo yenye kupotosha na kuleta taharuki yanayotolewa na watu wasiokuwa na nia njema.

Benki Kuu inautaka umma kupuuza matangazo na maelekezo yoyote kuhusu utoaji leseni au usajili wa watoa huduma ndogo za fedha ambayo hayajatoka mamlaka husika," alisema Prof. Luoga.

Alisema wananchi wanashauriwa kuwasiliana na mamlaka husika, iwapo wanakutana na changamoto mbalimbali katika mchakato wa maombi ya leseni au usajili wa huduma ndogo za fedha.

Desemba mwaka jana, BoT, ilitoa taarifa kwa umma kuhusu Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, iliyoanza kutumika rasmi tarehe Novemba Mosi, mwaka 2019.

Pia, taarifa hiyo ilisema Kifungu cha 57 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ambacho kinawataka watoa huduma ndogo za fedha wote kuwasilisha maombi ya leseni au usajili BoT, kwenye mamlaka kasimishwa katika kipindi cha miezi 12 mara sheria itakapoanza kutumika, Oktoba 31, mwaka huu.

Januari mwaka huu, BoT ilionya kuwa mtu yeyote atakayekutwa anatoa huduma hizo bila leseni atachukuliwa hatua za kisheria, na kwamba Kifungu cha 6 (1) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, kinakataza mtu yeyote kufanya biashara ya kibenki au kupokea amana kutoka kwa umma bila kuwa na leseni kutoka BoT.

### SERA HUDUMA ZA FEDHA

Aidha, Sera na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017, inaeleza kuwa lengo la huduma ndogo za fedha kwa wananchi hususan wa kipato cha chini ni kulinda watumiaji wa huduma hizo na kuwaondolea changamoto.

Katika sera hiyo, huduma ndogo za fedha zimeelezwa kuwa ni huduma zitolewazo kwa wananchi wa kipato cha chini, mtu binafsi, kaya au kikundi cha ujasiriamali.

Aidha, huduma hizo ni pamoja na mikopo ya karadha, fedha, nyumba ikiwamo huduma ya akiba, elimu ya fedha, bima na ujasiriamali.

Pia watoa huduma ndogo za fedha sera hiyo inawataja kuwa ni taasisi za huduma hizo, wakopeshaji binafsi watoa huduma hizo kidigitali, SACCOS, ikiwamo vikundi vya kijamii vya huduma hizo kama vile VICOBA, Upatu, VSLA na SILC.

# Kampuni ya kuchapisha karatasi za kura yatajwa

**Na Waandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema kuwa kampuni ya Ren-Form CC ya Afrika Kusini ndiyo iliyoshinda zabuni ya kuchapisha karatasi za kupigia kura.

Aidha, NEC imesema kulikuwa na ushindani katika mchakato wa kupata mzabuni na makampuni matatu yaliomba ambayo mengine ni Ellams Products Limited ya Kenya na Al Ghurair Printing and Publication LLC ya Dubai.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na umma na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, madai kuwa kampuni ya Jamana Printers ilipewa kazi hiyo hayana ukweli.

Alisema mchakato wote ulizingatia sheria na tangazo la fursa za zabuni la ujumla lilitangazwa kwenye tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) Julai 2, mwaka 2019 na kurudiwa Desemba 13, na kutangazwa tena katika moja ya magazeti ya serikali.

"Umma uliofahamishwa ni pamoja na viongozi wa vyama vya siasa, katika mpango wa manunuzi ya jumla ya zabuni 47 zilizoorodheshwa ilijumuishwa ya uchapishaji wa karatasi za kupigia kura. Njia ya kumpata mshindi iliyotangazwa ni ya ushindani wa wazi wa kimataifa," alifafanua.

Aidha, Dk. Charles alisema ufunguzi wa zabuni ulifanyika Aprili 14, mwaka huu...baada ya uchambuzi, mzabuni Ren-Form CC ilishinda.

Pia alisema kuwa vyama vyote vilishirikishwa katika Kamati ya Kitaifa ya Manunuzi na Lojistiki, na vilishiriki katika hatua zote za manunuzi ya vifaa vya uchaguzi katika dhana ya uwazi na ushirikishwaji.

Alisema vyama vingi ikiwamo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) havikuteuwa majina ya wajumbe wa kuandaa kamati ya kitaifa ya manunuzi na lojistiki licha ya kuandikiwa barua Juni 30, mwaka huu.

**Imeandikwa na Betrina Bishubo na Zainabu Ahmed, (SJMC)**


MEDICAL TEAMS International

**Procurement Opportunities**

Tender for Framework Agreements

Medical Teams International is Non-Government Organization (NGO) which was founded in 1979, providing life-saving medical care for people in crisis, such as survivors of natural disasters and refugees.

Medical Teams International, Kasulu Tanzania is inviting interested suppliers to express their interest to supply MTI with items per description below. All interested parties are invited to participate.

| | |
|---|---|
| **Procuring Entity:** | Medical Teams International |
| **Tender No:** | MTI20/GEN PROC/001 |
| **Tender Name** | Invitation to Tender for Framework Agreements |
| **Reference Number** | **CATEGORY A: SUPPLY OF GOODS** |
| PP/MTI-TAN/01/2020 | Supply of general stationery. |
| PP/MTI-TAN/02/2020 | Supply of office supplies. |
| PP/MTI-TAN/03/2020 | Supply and maintenance of photocopiers, scanners, computers, printers, Uninterruptible Power Supply (UPS), laptops, software, toners and other ICT accessories. |
| PP/MTI-TAN/04/2020 | Supply of branded items and promotional materials. |
| PP/MTI-TAN/05/2020 | Supply, installation and maintenance of fire and security alarms equipment and security systems. |
| PP/MTI-TAN/06/2020 | Supply of Fuel (Diesel & Petrol) |
| PP/MTI-TAN/07/2020 | Supply of bottled water, dispensing machines and maintenance. |
| PP/MTI-TAN/08/2020 | Supply of motor vehicle/cycle parts and accessories. |
| PP/MTI-TAN/09/2020 | Supply of airtime and scratch cards. |
| PP/MTI-TAN/010/2020 | Supply of office furniture's and fixtures. |
| PP/MTI-TAN/011/2020 | Medicines |
| PP/MTI-TAN/012/2020 | Medical Consumables |
| PP/MTI-TAN/013/2020 | Medical Equipments |
| **Reference Number** | **CATEGORY B: PROVISION OF SERVICES** |
| PP/MTI-TAN/014/2020 | Provision of catering services. |
| PP/MTI-TAN/015/2020 | Provision of air travel, reservations and ticketing services. |
| PP/MTI-TAN/016/2020 | Provision of sanitary, fumigation, pest control and cleaning services. |
| PP/MTI-TAN/017/2020 | Provision of internet services. |
| PP/MTI-TAN/018/2020 | Provision of hotel accommodation and conference facilities. |
| PP/MTI-TAN/019/2020 | Provision of security services (guards, dog patrols and security survey). |
| PP/MTI-TAN/020/2020 | Servicing, repair and maintenance of vehicles and motorcycles |
| PP/MTI-TAN/021/2020 | Vehicle Hire-minibus, pickups, hardtop Landcruiser's |
| PP/MTI-TAN/022/2020 | Provision of printing services |
| **Source of Fund** | Bureau of Population, Refugees and Migration & UNHCR |
| **Eligible Firms** | National (Registered in Tanzania) |
| **Method of Procurement** | National Competitive Bidding |
| **Mode Application** | Via Email; procurementtz@medicalteams.org (Please send an introduction email for document inquiry) |
| **Deadline** | 11th November 2020 4:30PM |
| **Bids Submission** | Effective 12rd October to 11th November 2020 |

*"Daring to love like Jesus, we boldly break barriers to health and restore wholeness in a hurting world"*

215940502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mtoto wa kike apewe msaada kufikia ndoto

**KILA** Oktoba 11 ni maadhimisho ya kimataifa ya mtoto wa kike, kwa mwaka huu kauli mbiu ni "Tumwezeshe mtoto wa kike, kujenga taifa lenye usawa" huku ya kimataifa ikiwa ni "sauti yangu, ni mustakabali wetu wa usawa".

Wakati siku hiyo ikiadhimishwa, kumekuwa na vikwazo vingi vinavyomkabili mtoto wa kike, na viliongezeka zaidi wakati wa corona, ambapo kwa kipindi cha miezi mitatu wanafunzi walichokaa nyumbani walijikuta katika mazingira magumu.

Utafiti uliofanywa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), ulibaini wakati wanafunzi walikuwa kwenye likizo hiyo unyanyasaji majumbani uliongezeka kwa kasi, jambo ambalo ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya mtoto wa kike.

Mkoani Shinyanga kwa mujibu wa Dawati la Jinsia kwa mwezi mmoja kati ya Machi na Aprili, wanafunzi 101 waliripotiwa kuwa na ujauzito ikiwa ni Shinyanga (26), Kishapu (25), Manispaa ya Shinyanga (20), Msalala (17) na Kahama (16).

Aidha, hivi karibuni katika Halmashauri ya Msalala wanafunzi 20 walipata mimba kwa kipindi cha Julai hadi Septemba.

Kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa changamoto ni kubwa hasa nyakati za mavuno ambapo wanafunzi huolewa kwa wingi. Kwa mikoa ya wafugaji kama Manyara na Arusha, watoto hukeketwa na kuandaliwa kwa ajili ya kuolewa kwa watu wa umri mkubwa.

Kimsingi, bado vikwazo vingi vinakuzwa na kusababishwa na jamii zetu. Mathalani, kila palipo na maslahi fulani basi mila na tamaduni hukumbukwa na kupewa kipaumbele katika maamuzi.

Hata hivyo, jitihada nyingi zinafanyika za kutoa elimu kwa jamii kuona madhara ya kumwozesha mtoto wa kike katika umri mdogo, hivyo kukatisha ndoto yake, lakini bado yapo matukio ya ukatili kama ubakaji, ulawiti na kunajisi.

Mathalani wiki iliyopita, Mahakama ya Hakimu Mkazi Lindi, ilimhukumu kifungo cha maisha jela kijana wa miaka 22, aliyemnajisi mtoto wa miaka mitatu wa shemeji yake, alipotakiwa kujitetea aliomba asipewe adhabu kali kwa kuwa alipitiwa na ibilisi wa mapenzi. Yapo mengi ya kujiuliza kwa mtoto wa miaka mitatu mtu anatafuta nini, huyo ibilisi wa mapenzi anampitia kiasi gani cha kumtamani mtoto wa umri huo?

Takwimu za matukio ya uhalifu dhidi ya watoto za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), zinaonyesha katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka 2016, jumla ya kesi 10,551 ziliripotiwa katika vituo vya polisi.

Kesi hizo ni kulinganisha na kesi 9,541 kwa kipindi hicho zikiwa ni za uhalifu wa ubakaji, ukeketaji wa watoto, wizi wa watoto, utekelezaji na mashambulio ya kudhulu mwili.

Aidha, Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF) linaleza watoto wa kike milioni 2 huolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 kila mwaka.

Haya yanatokea katika kipindi ambacho kuna ongezeko la matumizi ya mitandao ya kijamii, watoto wa kike wanadhalilishwa bila kujali kesho yao, kiasi cha wengine kufanya uamuzi mgumu ikiwamo kujidhulu.

Licha ya mapingamizi mbalimbali, bado Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ambayo inatambua mtoto wa kike, anaweza kuolewa kuanzia miaka 14 ikiwa wazazi wataridhia, huku Katiba ikimtambua mtu mzima ni kuanzia miaka 18.

Kwa ujumla mtoto wa miaka 14 hawezi kufanya maamuzi sahihi na hayuko katika utayari wa kubeba majukumu ya ndoa na viongo vyake kuzaa watoto na kuwalea.

Katika umri huo bado ni mtoto anahitaji kulelewa na kama alipata nafasi ya kusoma yupo darasa la saba, kidato cha kwanza au cha pili, anatakiwa kusoma ili atimize ndoto zake.

Ni wajibu wa jamii kumsaidia na kumwongoza njia sahihi mtoto wa kike, ili afanye maamuzi sahihi ya maisha yake ili awe kijana, mama na bibi mzuri atakayeleta mchango chanya kwa jamii yake.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ni Nyerere aliyepanda, kukuza mbegu elimu bora

**HISTORIA** ya elimu Tanzania Bara haiwezi kuzungumzwa bila kuutaja mchango wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere. Ndiye aliyeipitia na kuingalia mienendo na mifumo ya elimu ya Wajerumani, Waarabu na Waingereza, waliokuwa watawala zama hizo na kila kundi likibadili mfumo kulingana na matakwa yake bila kujali yale yaliyokuwa na manufaa kwa Watanzania.

Katika utoaji wa elimu, shule za mataifa mbalimbali zilitofautiana katika malengo, mitaala, sifa na taaluma za walimu, lugha ya kufundishia na ubora wa majengo ya shule na nyumba za walimu.

Tatizo kubwa zaidi lilikuwa ni ubaguzi katika utoaji wa elimu, kwa kuwa ilitolewa kwa wateule wachache, hasa kwa watoto wa machifu, viongozi wa dini na waliofanya kazi katika serikali ya kikoloni.

Lakini baada ya uhuru mwaka 1961, Mwalimu Nyerere alijitahidi kufuta ubaguzi katika utoaji wa elimu kwa kuondoa matabaka yaliyojengeka kwenye mfumo wa elimu wakati huo.

Mwalimu Nyerere alifanya hivyo, kwa sababu aliamini katika usawa na alihitaji mfumo wa utoaji wa elimu nchini kuwa sawa kwa wote, na serikali yake ikaanzisha mpango wa kuunganisha shule zote.

Lengo kuu lilikuwa ni kuwezesha watoto wa Kiafrika, Kizungu na Kiasia kusoma pamoja kwa lengo la kuondoa ubaguzi wa rangi, huku shule za kidini zikitaifishwa na kuwezesha watoto wengi zaidi kupata nafasi za kusoma.

Ni kutokana na mkakati wake wa kuboresha elimu nchini, Mwalimu Nyerere alianzisha elimu ya kujitegemea kwa lengo la kufanya vijana kuwa na uzalendo kwa taifa lao, kujitambua na kuwa majasiri na kuwa na bidii katika kazi.

Kimsingi, elimu ni moja ya mambo muhimu ambayo Mwalimu Nyerere aliyepa kipaumbele, katika siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, ambapo mwaka 1967 utekelezaji wake ulitimizwa rasmi baada ya kutangazwa Azimio la Arusha.

Kwa ujumla Mwalimu Nyerere aliitoa elimu ya Tanzania kutoka siku taifa lilipopata uhuru na kuifikisha kwenye ngazi hiyo, hivyo wakati huu wa kumbukumbu ya miaka 21 ya kifo chake, ni muhimu kuendeleza yale aliyofanya kwenye elimu ya nchi hii.

Kesho Oktoba 14 itakuwa imetimia miaka 21 ya kumbukumbu ya kifo chake, anakumbukwa kwa mengi aliyolifanyia taifa hili wakati wa uongozi wake, ili kuhakikisha linasonga mbele.

Miongoni mwake ni elimu ambayo aliitilia mkazo katika kuondoa ubaguzi na matabaka katika utoaji wa elimu nchini kwa lengo la kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anasoma bila kubaguliwa.

Lakini ilikuwa ni vita dhidi ya maadui watatu ujinga, maradhi na umaskini, ambayo upatikanaji wa elimu kwa wote ndiyo ilikuwa njia ya kummaliza adui ujinga na hivyo kuwa rahisi kuwamaliza maadui wawili waliosalia.

Juhudi za kumuenzi Baba wa Taifa kwenye uboreshaji wa elimu, zinaendelea kufanyika, hasa kwa utoaji wa elimu bure, ili hata watoto wa maskini waweze kusoma.

Kwa kiasi fulani baadhi ya familia zisizo na uwezo kiuchumi zilikata tamaa kutokana na kukosa fedha za kusomesha watoto kutokana na kuwapo kwa ada michango mbalimbali, hali ambayo ilikuwa ni kama ubaguzi.

Lakini sasa watoto wote wawe wa maskini ama matajiri, wanasoma bure kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha nne bila kuwapo kwa ubaguzi wa alienacho na asiye maskini.

Hata, kwenye utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, watoto wa maskini nao wanapewa kipaumbele ili kuhakikisha wanaipata bila usumbufu na kujiunga na kuendelea na masomo katika vyuo vikuu mbalimbali nchini.

# 70% moto wadhibitiwa Mlima K'njaro

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

Asilimia 70 ya moto ulioteketeza sehemu ya Mlima Kilimanjaro imedhibitiwa na vikosi vya watu zaidi ya 400 ikiwamo Jeshi la Polisi.

Moto huo ulizuka juzi jioni katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro na serikali kuongeza nguvu kwa kupeleka watumishi 170 wa Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka kukabiliana na moto huo.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, Angellah Nyaki, alisema moto huo umedhibitiwa baada ya vikosi hivyo kuongezwa.

Vilevile, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limesema linaendelea kuchukua tahadhari zote kuhakikisha usalama wa wageni na vifaa vyao, unaimarika bila kuathiri shughuli za utalii, ambazo zinaendelea kama kawaida, kwa njia ya Marangu iliyoathirika na moto huo.

Akizungumza jana kuhusu uamuzi wake wa kuwaondoa chuoni watumishi na wanafunzi wa chuo hicho kwenda kuokoa bionuai inayoendelea kupotea, Mkuu wa Chuo cha Wanyamapori-Mweka, Prof. Jaffari Kidegesho, alisema Mlima Kilimanjaro wanauchukulia kama maabara yao, hivyo hawawezi kukaa na kuona ukiendelea kuteketea.

"Sisi ni wadau muhimu sana wa mlima huu ambao kwetu ni kama maabara na tunautegemea kwa ajili ya mafunzo ya vitendo, kwa hiyo hatuwezi kukaa, wakati unaendelea kuungua.

"Nimepeleka watumishi 80 wa chuo na wanafunzi 90 pamoja na magari matatu makubwa na gari dogo moja kwa ajili ya kupeleka chakula, maji na shughuli nyingine ndogo za kiutawala."

Mara ya mwisho moto kama huo ulizuka katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro mwaka 2013.

Taarifa ya Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa TANAPA, anayeshughulikia mawasiliano, Paschal Shelutete ilisema moto huo ulizuka Oktoba 11, katika eneo la Whona, kituo cha kupumzikia wageni wanaotumia njia ya Mandara na Horombo.

Mpaka sasa moto huo umeteketeza idadi kubwa ya miti ya asili, makachero wanaofanya uchunguzi wa tukio hilo, bado hawajagundua chanzo cha moto huo.

"Moto unaendelea kudhibitiwa na vikosi vinavyoshiriki kuuzima katika eneo la Whona-Horombo. Vikosi vinavyoshiriki vinajumuisha wananchi, wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo na wa Chuo cha Mweka na Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji," alisema Kamishna Shelutete.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema mkoa wake umeomba msaada zaidi wa kupelekwa helikopta maalum ya kupambana na moto huo, wakati vikosi vya uokozi vikiendelea na juhudi za kuudhibiti.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha***

## Visiwa vya Ukara kupata usafiri wa uhakika

**Na Richard Makore,** MWANZA

TATIZO la usafiri kwa wananchi wa visiwa vya Ukara na Ukerewe mkoani Mwanza, linatarajia kubaki historia baada ya serikali kununua kivuko kipya cha MV Ukara kwa Sh. bilioni 4.2.

Kivuko hicho jana kiliingizwa majini baada ya kutengenezwa na kampuni ya Songoro Marine, jijini hapa na kitafanya safari zake kati ya kisiwa cha Ukara kwenda Ukerewe, mkoani Mwanza.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kuingiza kivuko hicho majini, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga, alisema kitakuwa na uwezo wa kubeba abiria 300, tani 100 na magari 10.

Kitafanya idadi ya vivuko kuwa 16 katika Ziwa Victoria ikiwa ni ahadi ya Rais John Magufuli.

Jumla ya Sh. bilioni 10 zimetumika kujenga vivuko mkoani Mwanza ili kuhakikisha wananchi wanaoishi katika visiwa 38 wanakuwa na usafiri wa uhakika.

Akizungumzia gharama za ununuzi wa kivuko hicho, Mwakalinga alisema kingenunuliwa nje ya nchi kingegharimu Sh. bilioni 22, lakini kampuni ya ndani ya Songoro Marine ilikubali kukitengeneza kwa Sh. bilioni 4.2.

Alitaja vivuko vingine vilivyonunuliwa miaka ya hivi karibuni kuwa ni pamoja na MV Ilemela na MV Chato.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Japhet Masele, alisema kwa sasa wana vivuko 30 ambavyo vinafanya kazi katika maeneo mbalimbali ya nchini.

Baada ya kivuko cha MV Ukara kuingizwa ziwani kitaendelea kufanyiwa mazoezi na kuhakikiwa na wataalamu.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, alisema wananchi wa Ukara sasa wamepata usafiri na kitakabidhiwa kwao hivi karibuni.

Tpb Bank
Grow with us

TAARIFA KWA WATEJA WETU
WA ILIYOKUWA BENKI YA TIB CORPORATE –
TAWI LA MWANZA

**Ndugu wateja,**
Tunapenda kuwajulisha wateja wa iliyokuwa Benki ya TIB Corporate Tawi la Mwanza lililoko katika Jengo la PSSSF Plaza Ghorofa ya Tatu kuwa tawi hilo litafungwa tarehe 30 Oktoba 2020. Wateja wote wa tawi hili wataendelea kupata huduma zote za kibenki katika matawi ya Benki ya TPB yaliyoko jijini Mwanza (Pamba, Kenyatta, Liberty) au katika tawi lolote la Benki ya TPB na mawakala waliosambaa nchi nzima.

***Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.***

**Kitengo cha Mawasiliano**
**Benki ya TPB Plc**
**Simu: +255 22 216294**

# Majaliwa: Dk. Mwinyi msafi na mwadilifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema nchi inahitaji rais atakayeunganisha Watanzania, kuwaletea maendeleo wananchi na kuzitunza tunu za taifa ambazo ni amani na utulivu.

Akiwanadi wagombea wa CCM katika mkutano wa kampeni, Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema kiongozi ambaye kazi yake kudanganya watu, kutukana, kuchonganisha, hafai na taifa linahitaji rais mchapakazi na mwenye uwezo wa kuzikusanya rasilimali za nchi pamoja na kuleta tija.

"Tunahitaji kiongozi ambaye ana uwezo wa kuisimamia serikali, wananchi hiki ni kipindi muhimu sana cha kufanya maamuzi," alisema.

Alisema nchi inahitaji kiongozi anayepambana na rushwa na ufisadi, awe msafi, mwadilifu na atakayeiongoza nchi na si mwingine ni Rais Dk. John Magufuli kwa Tanzania na Dk. Hussein Mwinyi kwa Zanzibar.

Alisema katika miaka mitano Rais Magufuli ameweza kuitunza tunu ya amani na kuleta maendeleo ya wananchi bila ya ubaguzi wa aina yoyote na kuwataka wananchi kumchagua tena ili kuiongoza nchi kwa miaka mitano ijayo.

Aidha, aliwataka wananchi kumchagua mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi ambaye ni mchapa kazi na mwenye uwezo wa busara za hali ya juu.

Aliwataka wananchi kutokubali kuuza vitambulisho vyao vya kupigakura, kwa sababu kuviuza ni sawa na kuuza utu na kukosa haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua kiongozi wamtakae.

Akizungumza katika mkutano huo, Dk. Mwinyi, alisema endapo atapata ridhaa ya kuiongoza Zanzibar atawawezesha wavuvi kuwa na zana za kisasa za uvuvi ili kazi zao ziwe na tija zaidi.

Alisema anafahamu kuwa hivi sasa kuna changamoto ya utitiri wa kodi ambazo wanatozwa wajasiriamali hivyo akiwa Rais atahakikisha anaondosha utitiri huo na kutakua na kodi ndogo ambayo itatumika mwaka mzima ili wafanye biashara yao bila ya bughuza.

Alieleza pia ataimarisha masoko ya kuuza bidhaa zao, kuwawezesha vijana kuajiriika katika uwekezaji na kupata mikataba ya ajira ili kunufaika na sekta ya utalii.

Pia, alisema ataondoa migogoro ya ardhi na wawekezaji, wakulima na wafugaji watakuwa na maeneo yao maalum kwa ajili ya kufanya shughuli zao bila ya kuathiri shughuli za wengine.

Alisema bado uvuvi haujawa na tija kwa sababu ya dhana duni walizonazo wavuvi Zanzibar hivyo atahakikisha anawapatia nyenzo za kisasa ili wavuvi kuvua katika eneo la bahari kuu.

Mgombea huyo pia alisema atahakikisha analinda mazingira ikiwamo kudhibiti ukataji mikoko ambayo husaidia kuhifadhi mazingira hasa mmong'onyoko wa fukwe.

Hata hivyo, alisema atapambana na udhalilishaji wa wanawake na watoto na matumizi ya dawa za kulevya hivyo alitaka jamii kuwa tayari kutoa ushirikiano kwa sababu wanaofanya vitendo vya udhalilishaji wanajulikana.



Kijiko cha kampuni ya Old South, kikichonga barabara ya Mtaa wa Tanesco, mjini Kisarawe, mkoani Pwani juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taulo zawakosesha masomo wasichana

**Na Zuwena Shame,** MKURANGA

UKOSEFU wa taulo za kike (sodo) shuleni umetajwa kuwa changamoto kubwa kwa wasichana Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani, ambayo inasababisha ufaulu wao kuwa duni.

Hayo yalibainishwa jana wilayani humo wakati wa hafla ya uzinduzi wa dawati la kuzuia ukatili dhidi ya watoto, sanduku la maoni na vyoo vya wasichana katika Shule ya Msingi Ngalawani.

Hafla hiyo inafanyika ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kilele cha Siku ya Mtoto wa Kike Duniani ambayo huadhimishwa kila Oktoba 11 ya kila mwaka duniani kote.

Akizungumza mbele ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Watoto Jinsia na Wazee, Dk. John Jingu, mmoja wa wanafunzi aitwaye Mwanamahawi Ayoub alisema kukosekana kwa taulo hizo zimekuwa changamoto inayosababisha washindwe kuhudhuria masomo yao ipasavyo.

Alibainisha kuwa baadhi wamekuwa wakilazimika kuomba ruhusa maalumu kukaa nyumbani wanapoingia mwezini, hivyo kukosa masomo na kusababisha kuwa na ufaulu mdogo ikilinganishwa na wavulana.

Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kalage alisema kuwa Shirika la HakiElimu lina mpango mkakati wa miaka mitano, ikiwamo kuelekeza mbinu na juhudi katika kupunguza mdondoko wa ufaulu kwa watoto wakike.

Dk. Kalage alisema kuwa moja ya changamoto walizozibaini katika utafiti na chanzo mojawapo kinachosababisha watoto wa kike kufeli kuwa, mazingira ya shule nyingi sio rafiki kama ukosefu wa taulo za hedhi, vyumba vya kujistiri na maji.

Alisema Hakielimu imewasaidia watoto wa kike wilayani humo kwa kuwapa ujuzi na vyerehani viwili ili kushona taulo hizo, ikiwa ni hatua ya kutafuta suluhisho.

Katibu Mkuu Dk. Jingu kwa upande wake alisema kuwa ulinzi kwa watoto ni jukumu la jamii nzima kuanzia familia, jamii na wadau mbalimbali wakiwamo walimu.

Aliwashauri walimu na wazazi kuhakikisha wanapata muda wa kuchunguza mienendo ya watoto na kujenga utamaduni wa kuzungumza na watoto wao, ili kubaini matatizo yanayowakabili ikiwamo ya ukatili wa kijinsia.

"Tunayo madawati zaidi ya 155 sehemu mbalimbali, madawati haya yatasaidia kuondoa vitendo vya ukatili na unyanyasaji na kuwajengea mazingira ya kusoma, kuwakinga dhidi ya ukatili," alisema Dk. Jingu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Mkuranga, Mhandisi Mshamu Munde, alisema Hakielimu inasaidia jitihada mbalimbali za elimu wilayani humo, ikiwamo kujenga vyoo vyenye matundu saba na chumba kimoja cha kubadilishia taulo.

# Mteule aahidi kuwakatia watoto bima ya afya

**Na Thobias Mwanakatwe**

DIWANI mteule wa kata ya Kitomondo, wilayani Mkuranga mkoani Pwani, Zuberi Salum, amesema atahakikisha anawalipia bima ya afya watoto wasiopungua 10 kila mwaka, ili kuhamasisha wananchi kuwakatia huduma hiyo kwa lengo la kuvifanya vizazi kuwa na afya njema.

Salum (pichani chini) ambaye amepita bila kupigwa, akizungumza katika mahojiano na gazeti hili jana, alisema atahakikisha zahanati zote zilizopo katika kata yake zinakuwa na mazingira bora kwa wafanyakazi na wagonjwa.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano amepanga kutekeleza vipaumbele vinne katika miaka mitano kwenye sekta ya elimu, afya, kilimo na maji kama chachu ya maendeleo.

Kwa upande wa sekta ya elimu, alisema atahakikisha anaboresha elimu kwa kujenga sekondari nyingine ili kuwapunguzia adha watoto kutembea umbali mrefu wa kilometa kumi kila siku, kufuata shule.

"Natumaini hii itakuwa chachu ya kuongeza nafasi ya ufaulu kwa wanafunzi na kuongeza watoto wengi, kujiunga na sekondari tofauti na hali ilivyo sasa," alisema Salum.

Kuhusu uhaba wa walimu kuanzia shule za msingi hadi sekondari, alisema litakuwa ni suala mtambuka katika vijiji vyote, atahakikisha anawashirikisha wadau na wananchi kuchanga pesa za kuongeza walimu wa ziada kuziba pengo la upungufu wa walimu kwenye baadhi ya shule zenye uchache.

Pia, atainua hali ya mwamko kwa wazazi na wanafunzi, kupenda elimu kwa kuwa baadhi yao hawana ari na elimu kwa kutokujua umuhimu wake na kusababisha kutofuatilia mahudhurio ya watoto wao wakiwa shuleni.



"Upande wa wanafunzi nitahakikisha kunakuwa na mpango maalumu wa kuwashindanisha wao kwa wao hasa walimu wapate motisha wa kazi zao, pindi wanapofanya vizuri katika mitihani yao ya mwisho ili waweze kuboresha elimu na kuinua kiwango kwa maendeleo ya kata," alisisitiza Salum.

Katika sekta ya maji alisema, atahakikisha anaboresha huduma hiyo katika kata nzima kwa kuwashirikisha wananchi, serikali na wadau kutatua tatizo hilo.

Alisema kwa sasa wananchi wengi wanapata maji kwa njia za kiasili ambazo sio salama na mikakati yake ni kuboresha ili adha hiyo iondoke.

Alisema ameshaanza kusaidia baadhi ya vijiji kupata huduma ya maji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa kuchimba visima virefu na vifupi na kuwaondolea adha ya kwenda umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

**SEKTA YA KILIMO**

Salum alisema kata yake imekuwa na fursa nyingi za kilimo ambazo zikitumika vyema zinaweza kuinua uchumi wa wananchi, iwapo ujuzi na ubunifu wa wataalamu utatumika vyema.

## Mkurugenzi akerwa watoto kuogeshwa dawa za mapenzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAIMU Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga Dk. Ntanwa Kilagwile, amesema anasikitishwa na kukerwa na baadhi ya wazazi ambao wamekuwa na tabia ya kuwapeleka watoto wao wa kike kwa waganga wa jadi kuwaogesha dawa za mvuto wa mapenzi.

Kilagwile aliyabainisha hayo wakati akizungumza na wazazi pamoja na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wa halmashauri hiyo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani ambapo kiwilaya yamefanyika katika viwanja vya shule ya Msingi Segese.

Alisema wanafunzi wanaogesha na kuchanjwa dawa za mvuto wa mapenzi ni wale wenye umri kati ya miaka 16 hadi 18 na hiyo imekuwa kisababishia kushindwa kufanya vema kwenye mitihani yao ya mwisho kutokana na kuwaza kuolewa baada ya kuoga dawa hizo.

"Sisi halmashauri tunalikemea sana jambo hili na ndio maana tunajenga mabweni ya watoto wa kike na mabweni manne kati ya sita tuliojenga yanatumia...hivi sasa tunatarajia kujenga shule ya sekondari kwa ajili ya wanafunzi wa kike kama moja ya kupamba na hili," alisema Kilagwile.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Neema Katengesya, alisema hakuna dawa ya kuondoa mikosi ya mapenzi, mikosi mingine inajitokeza pale mwanamke au binti anapokuwa anajipitisha kwa wanaume ili aitwe na kutongozwa.

## DC awataka wakulima korosho kumchagua JPM

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Selemani Mzee, amewahimiza wakulima wa korosho kuwa ifikapo Oktoba 28 wahakikishe kura zote wanampa mgombea urais wa (CCM), Rais John Magufuli, ili aendelee kuliongoza taifa.

Kauli hiyo aliitoa juzi wilayani Masasi mkoani hapa alipokuwa akizungumza na mamia ya wakulima wa korosho wa wilaya hiyo waliohudhuria mnada wa mauzo ya zao hilo.

Mzee alisema anawaomba wakulima hao kuwa wawachague wagombea wa udiwani na ubunge kutoka CCM.

Alisema siku ya uchaguzi wahakikishe wanakwenda vituoni na kupiga kura, wahakikishe wanajitokeza kwa wingi na kutimiza haki yao ya msingi ya kuwachagua viongozi wanaowataka.

Mzee alisema wakulima hao ili waendelee kupata maendeleo chanya kama ilivyo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita chini ya Rais Magufuli, waipe ridhaa CCM kwa kumchangua mgombea wa chama hicho kwa kura nyingi, ili aweze kushinda kwa kishindo.

Alisema kuna kila sababu ya kuwahimiza wakulima hao kumchagua mgombea huyo kwa sababu kwa kipindi cha miaka iliyopita amefanya mambo makubwa ambayo yameiweka nchi katika ramani nzuri ya dunia.

# TAFICO kurejea na fursa lukuki uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

UFUFUAJI wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), umetajwa kuwa utaiwezesha sekta ya uvuvi kuchangia katika uchumi wa taifa.

Kadhalika, imeelezwa kuwa ufufuaji wa shirika hilo ambalo lilianzishwa mwaka 1974 na kuwekwa katika mashirika ya kubinafsishwa chini ya Tume ya Rais ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma (PSRC) mwaka 1996, pia litatoa ajira kwa Watanzania.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Meneja Mkuu wa TAFICO, Ester Mulyila, na kueleza kuwa sasa wakati shirika likifufuliwa, lengo kubwa la serikali ni kuzifikia rasilimali zilizopo ukanda wa uchumi wa bahari (EEZ) pamoja na kunufaika nazo, badala ya kutegemea kuwapa leseni wageni kuvua samaki.

**Kuna mpango wa baadaye wa kununua meli nyingine kubwa ya kisasa ambayo inavua kwa kutumia vyavu, ingawa gharama yake ni kubwa.**

Mulyila aliwaambia wahariri wa vyombo vya habari waliotembelea eneo la shirika hilo Kigamboni jijini Dar es Salaam, kwamba hatua kadhaa zimeanza kuchukuliwa kuhakikisha shirika linaanza kuendesha shughuli zake.

Baadhi ya hatua hizo alizitaja kuwa ni serikali kuweka menejimenti sambamba na kuanzisha mchakato wa kutafuta vyanzo vya fedha za kuliendesha.

Kwa mujibu wa Mulyila, tayari menejimenti imeshakamilisha andiko la mpango wa biashara ambalo limeainisha miradi 10 ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 ijayo.

Moja ya miradi itakayotekelezwa ni kuwa na meli ya uvuvi katika ukanda wa kitaifa. Mradi mwingine ni wa kuvua kwa kutumia meli ya kisasa inayotumia ndoana.

Alisema meli hiyo inaweza kuwa tayari ifikapo katikati ya mwakani baada ya Japan kutoa ufadhili wa Sh. milioni 4.2 zinazojumuisha ununuzi na vifaa vyake, na kwamba itakuwa inavua ukanda wa uchumi wa bahari ikiwa na uwezo wa kuvua tani 35 kwa safari moja baada ya siku 30 ikiwa baharini.

Kadhalika, alisema kuna mpango wa baadaye wa kununua meli nyingine kubwa ya kisasa ambayo inavua kwa kutumia vyavu, ingawa gharama yake ni kubwa.

Miradi mingine iliyoainishwa kutekelezwa ni ufugaji wa samaki, uzalishaji wa vifaranga, uzalishaji wa chakula cha samaki, uzalishaji wa vizimba vya samaki, ufugaji samaki katika mabwawa pamoja na ujenzi wa viwanda vya samaki.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo yote utagharimu Sh. bilioni 82.9, huku akisema meli ya kwanza ya kisasa inatarajia kutoa ajira kwa Watanzania takribani 15,000.



Kaimu Meneja Mkuu wa Shirika la Uvuvi la Taifa (TAFICO), Ester Mulyila, akitoa maelezo kwa wahariri na waandishi wa habari walipotembelea maeneo ya shirika hilo Kigamboni jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Kikosi maalum chapunguza malalamiko ya mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limesema katika kipindi cha miezi minne ya uhai wa kikosi kazi cha dhararu kero na malalamiko juu ya uhifadhi wa mazingira, vimepungua na Watanzania wamejenga tabia ya kuona mazingira yanatunzwa na kulindwa.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alieleza jijini jana kwamba uanzishaji wa kikosi cha dharura kinachofanyakazi saa 24, umekuwa na manufaa kwa taifa kwa sababu wananchi wamepata mahali pa kupeleka taarifa na zikafanyiwa kazi.

"Hapo awali kulikuwa na malalamiko mengi kuhusiana na utiririshaji wa maji taka kutoka katika baadhi ya viwanda kwenda sehemu zisizohusika na wakati mwingine kwenye makazi ya watu. Lakini baada ya kuunda kikosi hiki kero zimepunguza sana hasa kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema mbali na kudhibiti utiririshaji wa majitaka kwenye maeneo yasiyoruhusiwa, kikosi kazi kimesaidia kudhibiti uchimbaji wa mchanga kando kando ya mito, kuthibiti uchafuzi wa kelele pamoja na ukataji miti kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

"Taarifa ambazo zimewasilishwa kwenye kikosi kazi zimesaidia sana kuchukua hatua za kudhibiti uchafuzi wa kelele, ukataji miti katika maeneo yasiyoruhusiwa na uchimbaji wa mchanga kando kando ya mito jambo linalochochea mafuriko na ubomokaji wa kingo za mito," alisema.

"Tayari NEMC imezihimiza halmashauri za wilaya kuhakikisha vijana wanahamasishwa kuunda vikundi na kuvisajili ili uchimbaji mchanga uratibiwe na halmashauri zipate ushuru," alisema.

Amesema udhibiti na uimarishaji wa tabia ya usafi wa mazingira katika makazi ya watu na mito vimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, hasa katika maeneo yenye watu wengi kama Jijij la Dar es Salaam.

# CUF Mtwara yapinga kusimamishwa kampeni

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

CHAMA cha Wananchi (CUF) Mkoa wa Mtwara kimekata rufani ya kupinga zuio la kusimamishwa kutofanya mikutano yake ya kampeni kwa siku 10 katika Jimbo la Mtwara Mjini yaliyotolewa na msimamizi mkuu wa uchaguzi wa jimbo hilo.

Msimamizi huyo alitoa zuio hilo Oktoba 10 kwa maelezo kuwa chama hicho kimekiuka maadili ya uchaguzi.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa CUF Mkoa wa Mtwara, Saidi Kulaga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na adhabu hiyo ya kufungiwa siku 10, bila ya kufanya kampeni.

Juzi Oktoba 10, msimamizi mkuu wa uchaguzi Jimbo la Mtwara Mjini, Kanali Emmanuel Mwaigobeko, alitangaza kuifungia CUF kufanya kampeni kwa siku 10 kwa kile kilichoelezwa kuwa chama hicho kimekiuka maadili ya uchaguzi.

**CUF haijaridhishwa na maamuzi hayo, na kwamba hawayatambui, kwa vile wanashindwa kufahamu makosa yao, hadi kupelekea kuchukuliwa hatua hiyo.**

Kulaga alisema CUF kimeshawasilisha barua ya rufani ya kupinga maamuzi ya kufungiwa kwa chama hicho kwa siku 10 kutokufanya kampeni katika Jimbo la Mtwara Mjini kwa madai ya kukiuka maadili ya kampeni.

Alisema CUF haijaridhishwa na maamuzi hayo, na kwamba hawayatambui, kwa vile wanashindwa kufahamu makosa yao, hadi kupelekea kuchukuliwa hatua hiyo.

Kulaga alisema CUF imeshtushwa na maamuzi hayo yaliyotolewa na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo, na kwamba hayajafuata kanuni na taratibu kwa vile yameangalia upande mmoja pekee kwa waliotoa malalamiko.

Alisema CUF tangu kuanza kwa kmapeni imefuata taratibu na kanuni zote za kampeni za uchaguzi na haijawahi kukiuka maadili ya aina yoyote kwenye kampeni zake, hivyo maamuzi hayo ya kufungiwa yamewashtusha.

Kulaga alisema wao CUF, wamekaa na kuona ni vema kuandika rufani na kuipeleka kwenye kamati ya maadili kupinga maamuzi hayo, yaliyotolewa na kutangazwa na msimamizi mkuu wa jimbo hilo, ambaye ni mwenyekiti wa kamati ya maadili ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ya jimbo hilo na kutaka kuiruhusu CUF kuendelea na mikutano yake.




Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri nchini (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampeni ya kuhamasisha programu ya uanagenzi kwa waajiri nchini pamoja na uzinduzi wa wiki ya huduma kwa wanachama. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shirika laiwezesha jamii kukabili vikwazo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SHIRIKA lisilo la Kiserikali la World Vision Tanzania Kanda ya Kati, limetumia zaidi ya Sh. milioni 30 katika kuihudumia jamii katika maeneo ya vijijini wilayani Kilosa Mkoa wa Morogoro, ili waweze kukabiliana na vikwazo mbalimbali.

Maeneo hayo ni Mtumbatu na Magoleni, huku vikwazo vikiwa ni upungufu wa madawati, bima ya afya kwa kaya maskini na ununuzi wa vyerehani 35 kwa vijana wahitaji.

Meneja wa World Vision Kanda ya Kati, Faraja Ulanga, alisema hayo katika risala yake kwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kilosa Yohana Kisitila, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye utoaji wa taarifa ya shughuli za kijamii zinazotolewa na taasisi hiyo katika kusaidia jamii katika nyanja za elimu, afya na ujasiriamali kwa vijana waliomaliza darasa la saba, ambao hakuweza kuendelea na elimu ya sekondari.

Ulanga alisema World Vision ilipokea maombi kutoka kwa jamii kupitia ofisi yako ya Magole kuhusiana na mahitaji na changamoto zilizopo katika jamii; kwamba kuna vijana wanaomaliza darasa la saba, lakini hawana ujuzi wala shughuli za ujasiriamali, hivyo wanahitaji vyerehani kwa ajili ya kuendesha shughuli za uzalishaji zinakazowaongezea kipato ndani ya familia zao, hivyo kujikwamua kiuchumi.

Pia alisema taasisi yake imeweza kutengeneza madawati 100, kwa Shule ya Msingi Mtumbatu, ili kuunga mkono juhudi za serikali za kusimamia sera ya elimu, bila malipo kutoka shule ya awali hadi sekondari kidato cha nne.

Aidha, alitaja eneo lingine ambalo taasisi hiyo imeshughulikia ni kuwakatia bima ya afya watoto wanaotoka katika familia yenye kipato kidogo 2,910, ili waweze kupata huduma ya matibabu bila ya vikwazo, kwa kuwa sera ya World Vision ni pamoja na kumsaidia mwanajamii kuwa na afya njema.

"World Vision tumeelekeza nguvu zetu kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali, ambapo leo tutawakabidhi vyerehani 35 kwa ajili ya kuwawezesha vijana katika shughuli za ujasiriamali, watoto 2,910 tumewakatia bima ya afya, madawati 100, kwa Shule ya Msingi Mtumbatu vyote hivi vina thamani ya Sh. milioni 31,475,000," alisema.

Kwa upande wake DAS Kisitila alishukuru Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kati kwa mchango wake katika jamii, kwamba serikali inatambua kazi nzuri zinazofanywa na wadau wa maendeleo ikiwamo taasisi hiyo, hivyo atatoa wito kwa mashirika mengine kuendelea kuihudumia jamii.

## Machinga watetea vitambulisho vyao

**Na Dotto Mwaibale,** IKUNGI

WAFANYABIASHARA wadogo katika Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, wamesema watu wanaovibeza vitambulisho vya wajasiriamali hawana uzalendo, na kuwa wanawashangaa wanaopotosha umuhimu wa vitambulisho hivyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wilayani hapa mwishoni mwa wiki, waliishukuru serikali kwa kuwapa vitambulisho hivyo ambavyo vimewafanya wawe huru na kuwa punguzia gharama kubwa iliyotokana na ulipaji wa ushuru mkubwa.

Mfanyabiashara wa matunda wa Kata ya Ihanja, Robert Christopher, alisema wapo huru baada ya kuanza kutumia vitambulisho hivyo.

"Sasa hivi adha ya kufukuzana na mgambo waliokuwa wakipita kudai ushuru haipo tena na zile Sh. 200 tulizo kuwa tukilipa ushuru kila siku ambapo kwa mwezi ilikuwa ni Sh.60,000 hazipo kwani tukilipa 20,000 hakuna malipo mengine kwa mwaka mzima," alisema Christopher.

Mama lishe, Pili Juma wa Puma, alisema tangu aanze kutumia vitambulisho hivyo amekuwa huru na akawataka wafanyabiashara wenzake kutodanganyika na wazushaji wanaodai vitambulisho kuwa havina tija.

## Waomba elimu kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Jovither Kaijage,** UKEREWE

WAKAZI wa Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza, wameomba serikali kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya serikali kuchukua hatua madhubuti hasa kwa kuelimisha jamii juu ya tatizo la mabadiliko ya tabianchi kama mkakati wa kukabili tatizo hilo, linaloendelea kuongezeka na kuleta madhara kwa watu na mali.

Rai hiyo ilitolewa jana na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bukongo na baadaye wakazi wa Kijiji cha Bukongo kwa nyakati tofauti waliohudhuria mafunzo ya kukabili tatizo hilo, yaliyotolewa na Shirika la Sauti ya Wanawake Ukerewe (SAWAU) kwa kushirikiana na Women Action Towards Economic Development (WATED) kwa ufadhili wa mashirika Global Alliance for Green and Gender Action na Both ENDs [GAGGA] ya Uholanzi.

Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bukongo, Emanuel Jovin, alipongeza hatua hiyo na kuahidi kuelimisha jamii inayomzunguka hasa juu ya tatizo la uharibifu wa mazingira, unaosababisha tatizo la tabianchi.

Alisema kama jamii itaelimishwa kwa kiwango cha kutosha, inaweza kushiriki kikamilifu kuendesha shughuli zake, kwa kuzingati ulinzi wa mazingira, hali ambayo itasaidia kupunguza madhara ya tabianchi kama vimbunga, ukame na magonjwa ya binadamu na mimea.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 13, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12

**Teknolojia mbadala ya zebaki inavyozua 'zogo'- 2**



Ukurasa 13

Watangaziwa bingo 'vipanga' kutalii Serengeti



Ukurasa 14

**'Wazee waambiwa kuanzia sasa hawatakufa kizembe'**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU, TABORA

# Tabora kuwa jangwa, chanzo kukata miombo

## ■Uharibifu watishia kukausha Ziwa Tanganyika

ONGEZEKO la ukataji miti, kilimo, kuchoma mkaa na ufugaji mkoani Tabora hususani Urambo na Kaliua, limechangia kutoweka misitu ya miombo yenye 'lindimaji,' na kuwa chanzo cha kushuka mno kiwango cha mvua hadi kuwa chini ya wastani uliokuwapo miongo kadhaa iliyopita.

Makala hii inayoandikwa kwa msaada wa Rainforest Journalism Fund na Pulitzer Center, inaeleza zaidi.

Kutokana na ukame kuna hatari wilaya za Urambo na Kaliua kuwa jangwa, licha ya jitihada kadhaa zinazofanywa na wadau kuidhibiti hali hiyo.

Shughuli za kukata miti ili kuandaa mashamba na kukausha tumbaku, kuchakata mbao, kuchoma mkaa ambao ni nishati mbadala wa umeme na gesi zinachangia kutoweka miti miombo.

Ofisa Misitu wa Wilaya ya Urambo, Jacob Mbeshi, anasema miti yenye ukubwa wa mita nane za ujazo inatumika kukaushia tumbaku iliyovunwa eneo la ekari moja inayokaushwa kwenye matanuru ya kisasa, wakati teknolojia ya kale inatumia miti zaidi.

Mkuu wa Idara ya Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Shadrack Yomba, anasema kabla ya mwaka 1990 maeneo mengi Tabora kama Urambo na Kaliua yalipata mvua kwa wastani usiopungua milimita 1,000, ikiwa ni matokeo ya kuwapo misitu mingi.

Anataja ongezeko la wahamiaji kwenye misitu ya wilaya hizo wakitokea Shinyanga, Mwanza, Simiyu, Geita na Kigoma, kuanzia mwanzoni mwa 1990, kiasi hicho cha mvua kimepungua kufikia chini ya wastani wa milimita 870 kwa mwaka.



Baadhi ya wakazi wa Urambo wakiangalia mti unaoteketea kwa moto kwenye Hifadhi ya Msitu wa Ulyankhulu mkoani Tabora, hivi karibuni. **PICHA ZOTE: VERONICA MAPUNDA**

Anasema hatua hiyo imesababisha kuwapo joto kuliko unyevunyevu kama ilivyokuwa kabla ya mwaka 1990.

Pia, mtaalamu huyo wa masuala ya mazingira anasema kumekuwapo upotevu wa mimea ya asili hasa isiyostahimili ukame kwenye maeneo hayo.

**KUHIFADHI MAZINGIRA**

"Kuna jitihada kadhaa za uhifadhi zinazofanywa na serikali kama kuhamasisha wakulima kupanda miti, lakini zinaathiriwa na kipindi kirefu cha jua kali kinachosababishwa na kutoweka kwa misitu," anasema Yomba.

Takribani asilimia 20 ya miti inayopandwa mashambani hukabiliana na ukame kwenye maeneo hayo ndiyo inayostawi na mengine hukauka anasema na kuongeza kuwa ukanda wa miombo unahusisha misitu iliyopo wilaya za Uvinza na Kibondo mkoani Kigoma, Mlele Katavi na mikoa ya Morogoro, Iringa, Lindi na Mtwara.

Mjumbe wa serikali ya Kijiji cha Igunguli wilayani Urambo, Eliud Luago, anasema miaka ya 1990, eneo hilo lilikuwa na mvua nyingi zilizochangiwa na kuwapo misitu ya miombo, lakini sasa ni kukame.

Aidha, anasema ardhi inapungua rutuba kutokana na kilimo cha tumbaku kinachohusisha ukataji miti kwa wingi na kwamba

kuna dalili za mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo yao, kama ilivyotokea msimu wa kilimo wa mwaka huu ambao kiwango cha mvua kilikuwa kikubwa na kuharibu mazao.

**MSITU UNATOWEKA**

Eneo linalotajwa kuathirika zaidi kwa ukataji ovyo wa miti ya miombo ni msitu wa Ulyankhulu uliopo wilayani Urambo, msitu huo wenye ukubwa wa hekta 229,600 ni miongoni mwa hifadhi za misitu ya wilayani humo inayojumuisha pia msitu wa Gereza la Kilimo Nsenda (hekta 2,380) na ile ya vijiji vya Kangeme, Itebulanda na Utenge -KIU ambacho ni kifupi cha majina ya vijiji hivyo, wenye hekta 846.5.

Awali, Halmashauri ya Urambo ilimiliki pia Hifadhi ya Msitu wa Ugala Kaskazini wenye ukubwa wa hekta 163,482.39 ambao umemilikishwa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Ofisa Misitu Mbeshi anasema ingawa umilikishwaji huo umechangia kupunguza mapato kwa Halmashauri ya Urambo na kuondoa fursa za uvunaji mazao ya misitu kama asali, lakini utachangia jitihada za uhifadhi wenye tija kutokana na TANAPA kuwa na weledi wa usimamizi na uhifadhi wa maliasili ikiwamo misitu.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Urambo (wakati taarifa za makala haya zikikusanywa), Sadoki Magesa, anasema asili ya msitu wa Ulyankhulu kuvamiwa na kugeuzwa makazi ya kudumu, kulitokana na kuingia kwa wahamiaji wakitafuta ardhi yenye rutuba na mvua za kutosha kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

Anasema waliongezeka huku wageni wengine walioingia wakijitwalia maeneo na kupanua shughuli za kilimo hasa cha tumbaku, mazao ya chakula na ufugaji.

Magesa anasema umuhimu wa msitu wa Ulyankhulu upo kwenye lindimaji ambalo hukusanya maji yanayoingia mito Ugalla, Igombe na Malagarasi, maziwa Nyamagono na Sagala hadi Ziwa Tanganyika.

Jarida la Umoja wa Mataifa, ukurasa wa mtandaoni wa ...stories.undp.org/lake-tanganyika-what-the-future-holds, ziwa Tanganyika ni miongoni mwa maziwa ya maajabu duniani, ni kongwe, lina kina kirefu barani Afrika, likitenganisha Burundi, Congo na Tanzania likinufaisha kiuchumi watu zaidi ya milioni 10.

Hifadhi ya msitu wa Mto Igombe uliopo wilayani Kaliua ni miongoni mwa maeneo yanayohitaji zaidi uoto wa miombo kutokana na kutegemea maji yanayotokea Ulyankhulu.

Hivyo, hatua ya wahamiaji kuingia na kuweka makazi kwenye hifadhi ya Ulyankhulu, inatarajiwa kuathiri pia upatikanaji mvua utakaochochea kukauka kwa vyanzo vya maji na kupotea kwa ekolojia ya eneo hilo.

Mratibu wa Wakala wa Huduma ya Misitu (TFS) wilayani Kaliua, Jackson Temu, anasema, Hifadhi ya Msitu wa Mto Igombe ilitokana na tangazo la serikali namba 32 la mwaka 1958, una ukubwa wa hektari 244,480 na ndicho chanzo kikuu cha maji ya bwawa la Igombe linalotumiwa na wakazi wa Manispaa ya Tabora na vijiji jirani.

INAENDELEA UK.12

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Teknolojia mbadala ya zebaki inavyozua 'zogo'- 2

BAADA ya kubaini athari za zebaki, Umoja wa Mataifa umeanzisha Mkataba wa Minamata, makubaliano ya dunia, kudhibiti na kusimamia uchafuzi utokanao na zebaki inayoishi muda mrefu katika mazingira, kusambaa na kuchafua mfumo mfuatano wa chakula (food chain).

Tanzania ina matumizi makubwa ya zebaki yanayohusisha wachimbaji wadogo, baada ya kuridhia mkataba wa Minamata, imetangaza sayanaid kuwa mbadala wa zebaki.

Hata hivyo, wachimbaji wana maoni tofauti wakipendekeza mengine kwa serikali, makala hii iliyoanza wiki iliyopita inaendelea na maoni yao.




Wachimbaji wadogo wakiwa kazini kwenye moja ya migodi mkoani Geita. **PICHA: IPP MEDIA**

**KUFANYIKE UTAFITI**

Mtendaji Mkuu (CEO) wa Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini (FEMATA) Hassan Kinega, akizungumza na Nipashe kuhusu mapendekezo ya sayanaid kuwa mbadala wa zebaki, anasema hawapingi kusitisha matumizi hayo ila wanachofahamu Minamata haielekezi kusitisha mara moja zebaki, ila inashauri kupunguza na baadaye kuiacha kutokana na athari.

Wachimbaji wanajua athari na wanafahamu namna bora ya badala yake wanashauri utafiti ufanyike zaidi kujua teknolojia bora na nafuu kwa wajasiriamali hao badala ya kukimbilia kwenye sayanaid.

Anasema wanafahamu kuwa uzalishaji wa zebaki unakwisha baada ya mzalishaji mkuu duniani China kuacha kutengeneza na kwamba huenda gramu moja ikawa ghali kuliko ile ya dhahabu.

Kinega anasema kuifanya sayanaid kuwa kemikali ya kuchenjulia dhahabu ni jambo gumu kwao kwani wanahitaji kuchimba, kusaga na kuchenjua dhahabu ili kuiuza na kupata fedha kwa muda mfupi ili kujikimu.

Anasema wanaweza kuchimba na kusaga virobo viwili mpaka vitano, kuvichenjua kwa zebaki na kuchoma kiasi wanachopata kiwe gramu moja au 10 ili kununua mahitaji kwa siku hiyo na kuendelea kuishi.

"Sayanaid inachukua siku saba kwanza kuna kuozesha dhahabu ndani ya visima na miundombinu mbalimbali inayohitaji mtaji mkubwa usiopungua Shilingi 3,000,000.

kuiweka, hizo mchimbaji mdogo hana."

Mtendaji Mkuu wa FEMATA, anasema sayanaid inahitaji tani nyingi za dhahabu si kama zebaki ambayo hukamata kiasi chochote ambacho mchimbaji atakuwa anachenjua.

**TEKNOLOJIA RAFIKI**

Kinega anapongeza hatua ya kujenga vituo vya mfano vya kuchenjua dhahabu kwa kutumia sayanaid vya Katente na Rwamugasa huko Geita, lakini anasema ili kutumia miundombinu yake mchimbaji anahitaji kuweka tani 100-300 za udongo wenye dhahabu kwenye miundombinu hiyo.

Ni kiasi kikubwa ambacho hawawezi kukusanya hivyo huenda ikawa vigumu mchimbaji mmoja mmoja kunufaika, licha ya kukiri kuwa sayanaid inakamta hadi asilimia 97 ya dhahabu kutoka kwenye udongo wakati zebaki inashika asilimia 30 na kuacha kiasi kikubwa mno.

"Kinachohitajika hapa ni utafiti wa mnyororo mzima wa uchimbaji na ukamataji wa dhahabu. Kuanzisha vituo vya taarifa za kimetreolojia kuhusu dhahabu.

"Metallurgical stations ziwepo kwenye migodi ili kupima mbale ('ores'), miamba na kuwaeleza wachimbaji namna bora ya kusaga udongo kwa kiwango gani ili kupata dhahabu?"

Anaongeza kuwa utafiti unahitajika kupata teknolojia rahisi na nyepesi ya kuvuna dhahabu si kukimbilia sayanaid yenye gharama kubwa.

Kukiwa na hizo stesheni wachimbaji watajulishwa namna bora ya kuchenjua, kusaga mwamba, kukusanya dhahabu nyingi kwa faida na kwa gharama nafuu.

Anasema taarifa za miamba ni muhimu kwa sababu mawe hutofautiana, mengine ni magumu na yanayohitaji pengine kusaga zaidi ili kuchimba dhahabu.

Aidha, kuna malaini kupindukia, hivyo utafiti utaeleza njia ipi ifanyike ikiwamo ya kuchuja dhahabu kwa kutumia maji na gunia mbinu inayofahamika kama 'gravitational'.

Kinega anaamini vituo hivyo vitatafiti na kushauri kuhusu kiasi cha maji na jinsi ya kuyamimina, ulalo wa chekecheo zinazotumiwa ili kupata matokeo bora kwa mfumo wa gravitational.

"Bila utafiti wa njia bora ya kuchenjua mchimbaji hawezi kufaidika na teknolojia ya sayanaid." Anaonya.

Anashauri Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO), la Madini la Taifa (STAMICO), Taasisi ya Geolojia Dodoma (GST) na Kituo cha Utafiti wa Madini Nzega kufanya utafiti huo ili kufanikisha utekelezaji wa Mkataba wa Minamata, lakini pia kuwanufaisha wachimbaji wadogo kwa kuwapa teknolojia mwafaka na tija.

Hata hivyo, ofisa mmoja wa madini katika Wizara ya Madini jina linahifadhiwa, anawashauri wachimbaji kubadilika na kuacha kupinga sayanaid bila sababu.

Akijibu hoja ya kuwa na vituo vya kutoa taarifa za miamba kuhusu miamba ya dhahabu, anasema ni vigumu kuwa na huduma hiyo kwa kila mgodi.

"Huwezi kuwa na bajeti ya kuhudumia utafiti wa miamba kile sehemu yenye dhahabu nchini. Kwanza madini hayo huonekana kwa muda mfupi. Wachimbaji huvamia, kuchimba na kuondoka siyo migodi ya kudumu tunaita 'gold rush.'"

Anawashauri kutafuta taarifa kwenye ofisi za madini za kanda zilizoko chini ya Tume ya Madini ili kujua taarifa za miamba.

Anasema hata hivyo wanaweza pia kufikisha mbale (ores) kwenye maabara ya GST au kwenye kanda na wakapata taarifa muhimu za dhahabu ndani ya sampuli walizochimba.

"Wengi hawataki kupeleka sampuli maabara na wanachong'ang'ania ni teknolojia ya zamani ya zebaki bila kujali kubadilika. Sampuli moja hupimwa kwa Sh. 50,000. Kwenye kiroba mchimbaji anaweza kupata gramu kadhaa pengine zaidi ya tano na gramu moja huuzwa zaidi ya Sh. 80,000 hivyo watumie utaalamu na kubadilika si kulalamika."

Anasema wachimbaji hao wanapewa elimu za kuchenjua, wamejengewa vituo vya mfano vya Katente na Rwamugasa, kuna vijarida, mafunzo na wanafundisha kuhusu miamba na namna bora za kupata madini hivyo wabadilike na kuanza kufikiria kutumia sayanaid badala ya kulalamika.

# TABORA KUWA JANGWA, CHANZO KUKATA MIOMBO UHARIBIFU WATISHIA KUKAUSHA ZIWA TANGANYIKA

INATOKA UK.11

Vilevile, anasema msitu huo una ardhi oevu ya Malagarasi inayohudumiwa na kusimamiwa na TFS katika wilaya za Kaliua, Uyui na Nzega mkoani Tabora.

Ofisa Miti wa Wilaya ya Kaliua, Bucheye Wambura, anasema, karibu kila eneo limechukuliwa na wahamiaji waovuna miti na rasilimali nyingine wanavyotaka na kusababisha ugumu wa usimamizi.

**ATHARI KIIKOLOJIA**

Ofisa Misitu wa Wilaya ya Urambo, Jacob Mbeshi, anasema athari nyingine za kuharibu mazingira ni kupotea miti muhimu kama mninga ambayo kamati ya wilaya ya uvunaji iliweka zuio la kuivuna. Aidha, mti wa mkurungu ni miongoni mwa inayovunwa ovyo na kuharibu uoto wa asili wa miombo.

**WANYAMAPORI**

Kwa upande mwingine, uharibifu wa misitu hiyo unatajwa kuwa chanzo cha kutoweka kwa wanyamapori ambao awali, walipatikana kwenye maeneo kadhaa.Wanyama hao ni tandala, kongoni, palahala, tohe, simba na twiga.

Wenyeji wa maeneo ya karibu na msitu wa Ulyankhulu wanasema, wanyama hao walihamia msitu uliopo Igombe na kuelekea Hifadhi ya Kigosi.

Shuhuda nyingine za wenyeji zinaeleza kwamba kuna nyakati simba wamekuwa wakitokea Kigosi walipotorokea, na kurejea Ulyankhulu kupitia eneo wazi linalosababishwa na kukata miti hadi Ugala, hatua inayoelezwa kuwa kuna hatari ya watu na mifugo kushambuliwa na wanyama hao.

**MIFUGO NA UKAME**

Kishike Darushi, mfugaji aliyekuwa akilisha mifugo kwenye Hifadhi ya Msitu wa Ulyankhulu, anasema kuna ukame unaosababisha watembee umbali kusaka maji na malisho, aidha hakuna kivuli kutokana na kukata miti ovyo na wafugaji huchomwa na jua muda wote.

**WAVAMIZI KUSAJILIWA**

Licha ya kudaiwa kuvamia na kuweka makazi, wahamiaji hao walifanikiwa kusajili makazi yao na kupata hadhi ya vijiji rasmi, wakifikishiwa huduma za kijamii kama shule, zahanati na umeme, ingawa baadaye, vyeti vya usajili vilirejeshwa kwenye halmashauri husika ili kufanyiwa uhakiki.

Vijijini vilivyopo Ulyankhulu na kata zake kwenye mabano ni pamoja na Ukwanga na Mlangale (Songambele), Unzali, Uyogo, Igunguli, Milambo, Igembensabho na Kasela (Uyogo).

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Magesa aliliambia Nipashe hivi karibuni kuwa Ulyankhulu ni miongoni mwa misitu iliyotangazwa hivi karibuni na serikali, kutumika kwa makazi na shughuli za kibinadamu.

"Tumepata taarifa ya serikali kuruhusu vijiji hivyo kuendelea kuwapo, lakini bado hatujapewa barua rasmi ya kiofisi," Magesa anasema. Mwenyekiti wa Kijiji cha Igunguli ambacho ni miongoni mwa vilivyomo kwenye hifadhi hiyo, Lucas Lala, anasema kaya zenye takribani watu 6,545 kijijini humo wanatambua kuwa eneo hilo ni halali kwa makazi na shughuli za binadamu.

**URASIMISHAJI MISITU**

Kwa mujibu wa Ofisa Misitu wa Wilaya ya Urambo, Jacob Mbeshi, urasimishaji misitu ni utekelezaji wa mradi wa miombo, uliofanyika kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Global Environment Facility (GEF).

ELIMU
## NA SABATO KASIKA

# Watangaziwa bingo ‘vipanga’ kutalii Serengeti

## ■Shule bora kitaifa kula 3,000,000/- papo hapo

NDIYO ufunguo wa maisha tena unatajwa kuwa ni msingi wa maendeleo. Wengine huitaja kuwa ni kila kitu, hiyo ndiyo elimu na kila mmoja anashauri ‘kumshika sana elimu usimwache aendezake’.

Ndicho kinachomsukuma Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Antony Mtaka, kutangaza mbinu kadhaa zikiwamo fedha na safari za kiutalii kwenye hifadhi kwa walimu watakaofaulisha wanafunzi kwa viwango vya alama za A.

Simiyu ni miongoni mwa mikoa yenye mikakati mbalimbali ya kuboresha elimu katika shule za msingi na sekondari, ili kushika nafasi za juu kimkoa na hata kitaifa kwenye matokeo ya mitihani.

Motisha kwa wanfunzi na walimu ni miongoni mwa mikakati hiyo inayowekwa na wadau wa elimu, ili kila upande uweze kutimiza wajibu inavyotakiwa, hatimaye lengo la kuboresha elimu mkoani humo litimie.

Mkuu wa Mkoa Mtaka, katika mazungumzo yake na gazeti hili, wakati akielezea zawadi zilizoandaliwa na mkoa kwa wanafunzi watakaofanya vizuri mtihani wa taifa wa darasa la saba.

Mtaka anataja zawadi hizo ambazo pia zitawahusu walimu kuwa ni pesa taslimu na utalii wa ndani kwa walimu, katika mbuga za Serengeti kama njia mojawapo ya kuwatia moyo ili waendelee kufundisha kwa bidii na hamasa.

“Kabla ya mtihani nilizitembelea shule za msingi Somanda A na B pamoja na Sima A na B za mjini Bariadi kwa lengo la kujiridhisha na maandalizi ya mtihani na kuwatakia heri wanafunzi watakaofanya mtihani huo,” anasema Mtaka.

Wanafunzi wamedhamiria kushika nafasi ya kwanza kitaifa katika mtihani huo kwa kuwa mikakati ya taaluma iliyopo na maandalizi yaliyofanyika, vinawawezesha kufanya hivyo, anasema Mtaka.

### MGAWANYO WA ZAWADI

Mkuu huyo wa mkoa anafafanua kuwa wanafunzi watakaoingia 10 bora kitaifa kila mmoja atazawadiwa Sh. 500,000, na mwalimu atakayeongoza kwa ufaulu wa kupata alama nyingi za A kimkoa kwa kila somo atazawadiwa Sh. 500,000.

“Shule itakayoingia 10 bora kitaifa itapewa Sh. 3,000,000, wilaya itakayoingia 10 bora walimu wake wataenda kufanya utalii wa ndani katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti,” anasema Mkuu wa Mkoa.

Anaongeza kuwa, katika matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka 2019, Simiyu ilitoa wanafunzi wanne walioingia 10 bora kitaifa kwa shule za serikali na kila mwanafunzi alizawadiwa Sh. 300,000.

“Ninawashukuru walimu wa Simiyu kwa kazi nzuri wanayoifanya, viongozi na watumishi wengine toeni kipaumbele kwao katika maeneo ya huduma ili wapata nafasi ya kuwafundisha wanafunzi,” anasema.



Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, akizungumza na wanafunzi kabla ya Mtihani wa Taifa wa darasa la saba uliofanyika wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

Aidha, jumla ya wanafunzi 30,779 wiki iliyopita walifanya mtihani huo wa taifa wa darasa la saba, huku akibainisha kuwa maandalizi yaliyofanywa na walimu, wazazi, viongozi na wadau wote wa elimu yanawapa matumanini.

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu wa Mkoa, Ernest Hinju, azma ya mkoa ni kushika namba moja kitaifa na kwamba ndiyo matokeo wanayotarajia.

“Mkoa wa Simiyu una shule za msingi za 549 zikiwamo 13 za binafsi, sekondari ni 158, za binafsi ni 12 ,” anasema Hinju.

### KAMBI ZA KITAALUMA

Mwaka 2017 Simiyu ilianza mikakati ya kuboresha elimu kwa kuanzisha kambi za kitaaluma, ambazo zinatajwa kuwa zimeendelea kuongeza ufaulu kwa wanafunzi kwa wanafunzi, anasema Hinju.

Wazo la kuanzishwa kwa kambi hizo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa huo Mtaka, ingawa anaelezwa kuwa, mwanzoni mwa utekelezaji wake hazikupokelewa vizuri na wadau, anasema Mtaka.

Walianza na kambi za wanafunzi wa kidato cha sita pekee, huku kukiwa na changamoto za kukosekana kwa mahitaji muhimu kwa wanafunzi wa kike, lakini hawakukata tamaa anaongeza.

> “Ninawashukuru walimu wa Simiyu kwa kazi nzuri wanayoifanya, viongozi na watumishi wengine toeni kipaumbele kwao katika maeneo ya huduma ili wapate nafasi ya kuwafundisha wanafunzi,” anasema.

“Kwa kipindi hicho wanafunzi walikaa kambini kwa muda wa wiki mbili na bado hakukuwa na matokeo mazuri, kwani mkoa ulishika nafasi ya 29 kati ya mikoa 31 matokeo ya kidato cha sita mwaka 2017,” anasema Mataka.

Anaeleza kuwa mwaka 2018 wanafunzi wa kidato cha sita waliwekwa kambini tena kwa muda wa siku 30, ndipo mafanikio yakaanza kuonekana kwa mkoa kushika nafasi ya 10 kitaifa kwa mara kwanza.

“Mafanikio hayo yalianza kubadilisha mawazo ya baadhi ya watu waliokuwa wakipinga kambi hizo, kwani wanafunzi wa kidato cha nne nao walianza kambi kwa siku 30,” anasema Mkuu wa Mkoa.

Kambi hizo zilizidi kuzaa matunda, kwa vile mkoa uliingia 10 bora kwa mitihani yote miwili ya kidato cha nne na cha sita na kuanzia hapo ikawa ni ajenda kuu kwa kila mdau wa elimu mkoani humo.

“Mwaka 2019, matokeo ya kidato cha nne, mkoa wa Simiyu ulishika nafasi ya tano kati ya mikoa 31, ukitanguliwa na mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Iringa na Njombe,” anasema.

Anasema, anaamini kwamba, hata wanafunzi waliofanya mtihani wa taifa wa darasa la saba wanaweza kuibuka na matokeo mazuri, kwa madai kwamba wameandaliwa vizuri kwa ushirikiano wa wadau wote wa elimu.

### HISTORIA YA SIMIYU

Mkoa wa Simiyu ulianzishwa kwa Tangazo la Serikali (GN) Na. 72 Machi 2 , 2012, ukiwa na wilaya tano za Meatu, Itilima, Maswa, Busega na Bariadi, taraifa 16, kata 130, vijiji 471 na mitaa 92.

Ofisa Elimu Hunji anasema, Simiyu imegawanywa kutoka mkoa wa Shinyanga, na kwamba wakati huo mkoa huo ulikuwa wa mwisho kielimu na hasa wilaya ambazo sasa ziko Simiyu.

“Baadaye kutokana na juhudi za viongozi wa mkoa na wadau wa elimu, ulianza kubadilika na sasa unazidi kubadilika kwani matokeo ya mwaka jana kidato cha sita umeshika namba tatu kitaifa,” anasema.

Anasema, mwaka jana, matokeo ya kidato cha nne mkoa ulishika namba saba kitaifa na darasa la saba wakawa namba nane na anajigamba kuwa mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka huu, wanaweza kushika namba nzuri zaidi.



ELIMU

NA MARCO MADUHU, KAHAMA

# 'Wazee waambiwa kuanzia sasa hawatakufa kizembe'



Wazee wilayani Kahama kwenye mkutano wa kujadili changamoto na kuzitafutia ufumbuzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

WAZEE wilayani Kahama wameambiwa kuanzia sasa hawatakufa kizembe kutokana na kukosa dawa na vipimo kitu ambacho ni haki yao. Sera ya Wazee ya mwaka 2003 inamtaja mzee kuwa ni yule mwenye umri wa zaidi ya miaka 60, ambaye anahitajika kupatiwa huduma ya matibabu bure na pia anaaminika kuwa hana kipato, hivyo wala hana nguvu za kufanya shughuli za kumwingizia kipato.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Kitaifa la Kutetea Haki za Wazee (Help Age) na serikali, walibaini kuwa asilimia 96 ya wazee Tanzania Bara, wanakabiliwa na maisha magumu kutokana na kutokuwa na ajira rasmi yenye kiinua mgongo, huku asilimia nne ndiyo walikuwa na ajira.

Kutokana na idadi kubwa ya wazee kukabiliwa na ugumu wa maisha, wamekuwa wakiandamwa na changamoto mbalimbali hasa za kufikia matibabu, licha ya wengine kuwa na vitambulisho vya msamaha wa matibabu, lakini wamekuwa wakiambulia kupimwa na kuambiwa wakajinunulie dawa.

Aidha, utafiti unaonyesha kuwa wengi wametelekezewa wajukuu na watoto wao ambao wamekimbilia mijini na hivyo kuwafanya wazee kuendelea kukabiliwa na ugumu wa maisha zaidi, sababu ya kuwa na familia kubwa, huku wakiwa hawana nguvu tena ya kufanya kazi za kuwaingizia kipato.

Baraza la Wazee Wilaya ya Kahama baada ya kuona wazee wanakabiliwa na changamoto ya kupata huduma za matibabu, wakabuni mbinu ya kuanza kuandika maandiko ya kuomba msaada wa kukatiwa bima za afya iliyoboresha (CHF) na kuyapeleka kwenye halmashauri, wadau mbalimbali, pamoja na taasisi za kidini.

Katibu wa baraza hilo, Underson Lyimo, anasema katika Halmashauri ya Kahama Mji kuna wazee 6,792, wanawake ni 2,793 na wanaume 3,999, ambao kwa mwaka wa fedha (2019-20), waliwakatia bima ya afya wazee 3,380, fedha zilizotolewa na halmashauri, wadau, pamoja na taasisi za kidini.

Anasema kwa mwaka huu wamewakatia tena bima ya afya wazee 1,388 fedha zikitoka halmashauri, wadau, pamoja na taasisi za kidini, ambazo zitakuwa msaada wao mkubwa wa kupata matibabu bure ya uhakika pamoja na kuhudumia wajukuu zao wasiozidi watano.

Elizabeth Elias ni mzee, anayesimulia namna bima ya afya CHF iliyoboreshwa jinsi ilivyookoa maisha yake, kuwa alikuwa akikabiliwa na matatizo pamoja na uvimbe mguuni na alikuwa hana fedha ya matibabu, lakini bima hiyo iliokoa maisha yake na sasa ana hali nzuri.

Anasema awali kabla hajapata bima hiyo ya afya, alikuwa akipata shida ya matibabu sababu ya ukosefu wa fedha, ambapo alipokuwa akienda hospitali kupata huduma alikuwa akiambulia kupata vipimo, pamoja na dawa za maumivu Panado, huku dawa zingine akiambiwa akanunue, na kuamua kutumia mitishamba sababu ya kukosa fedha.

"Nashukuru sana kupata bima hii ya afya, ambayo imekuwa mkombozi mkubwa sana wa maisha yangu, nimekuwa nikipata huduma ya matibabu bure kabisa pamoja na dawa, na sasa hali yangu imeimarika,"anasema Elias.

Sada Mkumbi ni mzee anayeishi na wajukuu zake wanne, ambao anasema walitelekezwa na watoto wake waliokimbilia Dar es Salaam na Zanzibar, anasema anaishi na wajukuu hao peke yake na babu yao alishafariki dunia na awali kabla ya kupata bima ya afya alikuwa akishindwa kuwapatia matibabu.

Anasema hana kazi ya kumwingizia kipato ambapo ameshazeeka na wajukuu zake bado ni wadogo wanasoma shule, lakini linapofika suala la kuwapatia matibabu alikuwa anashindwa kutokana na ukosefu wa fedha, lakini baada ya kupata bima hiyo ya afya, hana wasiwasi tena ambapo wamekuwa wakipata matibabu bure.

"Uzuri wa kadi hii ya bima ya afya ina hudumia watu sita wa kaya moja, na mimi katika familia yangu tupo watu watano, hivyo tunapata huduma ya matibabu bure pamoja na wajukuu zangu, na shukuru sana wadau ambao wametupatia msaada wa bima hizi pamoja na halmashauri," anasema Mkumbi.

Mchungaji wa Kanisa la Mito ya Baraka wilayani Kahama, Richard Mlema, anasema kanisa hilo limeguswa na baada ya kuona wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa matibabu, na kuamua kuchangisha fedha na kutoa kadi za bima ya afya CHF kwa wazee 70.

"Kanisa la Mito ya Baraka tutaendelea kushirikiana na wadau wengine, pamoja na serikali, kutatua changamoto ya wazee hasa kwenye huduma ya matibabu, eneo ambalo ni la muhimu sana sababu linagusa maisha ya mtu," anasema Mchungaji Mlema.

Jonathani Shayo, ni Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Kahama Mji, anasema wamekuwa wakitenga bajeti ya wazee kila mwaka wa fedha, kwa ajili ya kuwakatia bima za afya wazee ili kuwarahisishia upataji wa matibabu bure.

Anasema kwa mwaka wa fedha (2019-2020) walitenga Sh. milioni 11.7 kwa ajili ya kuwakatia bima ya afya wazee, ambapo kwa mwaka wa fedha (2020-21) kutokana na ufinyu wa bajeti, wametenga Sh. milioni sita na tayari wameshawakatia wazee 1,200 bima hiyo ya afya CHF iliyoboreshwa.

"Halmashauri ya Kahama Mji tutaendelea kutenga bajeti kila mwaka wa fedha kwa ajili ya kuwakatia bima za afya wazee, pamoja na wengine kuwapatia vitambulisho vya msamaha wa matibabu bure, ambapo kwa takwimu wazee wenye vitambulisho hivyo wapo 303 na lengo ni kuhakikisha tuna waenzi wazee wetu kwa vitendo," anasema Shayo.

Lukas David, akimwakilisha Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kahama, anawatoa wasiwasi wazee kuwa serikali itaendelea kuwaboreshea huduma za matibabu hasa kwenye upatikanaji wa dawa za magonjwa ya wazee, ambapo suala la kuwatengea dirisha lipo pamoja na daktari wa magonjwa yao.

Anasema kwenye huduma za afya zahanati na vituo vya afya, kuna baadhi ya dawa huwa hazipo maeneo hayo kutokana na kiwango cha utoaji tiba, hivyo wazee wakiambiwa dawa hazipo wanapaswa kwenda hospitali ya wilaya kupatiwa dawa, ili kuondoa changamoto ya kuambiwa wakanunue.

Katibu wa Umoja wa Wazee Wilaya ya Kahama (UWAKA), Paulo Ntelya, anakazia suala la upatikanaji wa dawa kwa wazee kwenye huduma zote za kiafya, ili kuondoa usumbufu wa wazee kuambiwa wakanunue dawa na kuamua kurudi nyumbani kwa kukosa tiba sahihi.

"Natoa wito kwa serikali suala hili la upatikaji wa dawa kwa wazee kwenye maeneo yote ya huduma za afya ni muhimu sana, huwezi kumwambia mzee afuate dawa kwenye hospitali ya wilaya na wakati ni mbali na ukimwambia mzee arudi nyumbani hakuna dawa au akanunue ni sawa na kumkejeli asubiri kifo," anasema Ntelya.

Winnie Hinaya Ofisa Miradi wa Shirika la Kutetea Haki za Wazee Mkoa wa Shinyanga, anasema halmashauri zote sita za mkoani humo, zinapaswa kuiga mfano wa Halmashauri ya Kahama Mji, kutenga bajeti kila mwaka wa fedha na kuwatia bima ya CHF ambao zitawasaidia kupata matibabu kwa urahisi.

Anasema shirika hilo la kutetea haki za wazee, linaendesha miradi ya kushawishi halmashauri kutenga bajeti kila mwaka wa fedha, kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wazee likiwamo suala la matibabu, na kuipongeza Halmashauri hiyo ya Kahama Mji kwa kuwajali wazee.



# Majosho 511 yakarabatiwa kudhibiti magonjwa ya ng'ombe

**Na Augusta Njoji,** BAHI

SERIKALI imekarabati majosho 511 nchini katika mwaka 2019, ili kutokomeza vifo vya ng'ombe vinavyotokana na magonjwa yanayoenezwa na kupe.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na wafugaji wa Wilaya ya Bahi, kwenye kampeni ya uogeshaji mifugo, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, alisema pamoja na ukarabati huo pia imejenga majosho mapya 78.

"Hatua ya uogeshaji mifugo imesaidia kupungua vifo vya ng'ombe hususan ndama kwa asilimia 30 ukiogesha hakika vifo vya ng'ombe tutatokomeza," alisema.

**Hatua ya uogeshaji mifugo imesaidia kupungua vifo vya ng'ombe hususan ndama kwa asilimia 30 ukiogesha hakika vifo vya ng'ombe tutatokomeza.**

Prpf. Nonga alisema kwa mwaka 2020 lita 15,600 za dawa zimenunuliwa na tayari kusambazwa kwenye halmashauri 162 zenye majosho yanayofanya kazi 1,967 ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka jana.

"Takribani lita 4,000 zimeongezeka na majosho pia yameongezeka, kwa Wilaya hii ya Bahi zimekabidhiwa lita 126 za dawa ya kuogeshea mifugo," alisema.

Alieleza kuwa dawa hiyo itatumika kwenye majosho 20 ya wilaya hiyo na kwamba kutokana na kuwa ni wilaya ya kimkakati wizara itaendelea kutoa dawa baada ya kukamilisha kukarabati majosho mengine.

"Tumeamua Wilaya ya Bahi iwe ya mfano mtu akitaka kuja kujifunza udhibiti wa magonjwa ya mifugo basi aje Bahi, wanafanya vizuri sana kwenye uogeshaji na chanjo na hii ni kinga kubwa mbili dhidi ya magonjwa ya mifugo,"alisema.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bahi, Dk. Fatuma Mganga, alisema baadhi ya miundombinu ya mifugo ni ya muda mrefu hivyo kazi ya ukarabati inaendelea.

Alisema wilaya ina mahitaji ya majosho 24 na yaliyopo ni 22 ambapo kati yake manne hayafanyi kazi.

Pamoja na hayo, Dk. Mganga alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kupunguza mifugo ili iendane na eneo lililopo kwa ajili ya ufugaji.

"Eneo linalofaa kwa ajili ya malisho ni hekta 133,156, kulingana na uwiano wa kitaifa ambao ni mnyama mmoja kwa hekta 2-3 kwa mwaka, eneo hili linatosheleza ng'ombe 44,385 huku ng'ombe waliopo ni 294,235, eneo halitoshi kulingana na mifugo iliyopo," alisema.



Mwendesha bodaboda na abiria wake wakijaribu kuinyanyua pikipiki baada ya kupata ajali, eneo la Chang'ombe, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waliojimilikisha maeneo ya umma wapewa angalizo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Josephat Maganga, amewaonya watu waliojimilikisha maeneo ya umma kuachia maeneo hayo haraka kabla hawajachukuliwa hatua za kisheria.

Maganga aliyasema hayo juzi alipokuwa kwenye ziara Kata ya Chahwa jijini hapa kwa ajili ya kusikiliza kero.

Alisema maeneo hayo ni pamoja na masoko, shule, mabwawa na mengine.

Mkuu huyo alisema kuna sheria mbalimbali za ardhi na hakuna mtu aliye juu ya sheria hizo kwa kuwa zimewekwa kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania.

Alisema maeneo yaliyotambuliwa kwa matumizi ya umma kama soko, mabwawa, mpira, gulio la ng'ombe na lambo la serikali kuna watu wamejimilikisha ni vyema wakapisha kabla ya kuchukuliwa hatua.

"Maeneo ambayo watu walijimilikisha waondoke mara moja hivi tukitaka kuwekeza tutakwenda kuwekeza bila matatizo," alisema Maganga.

Alisema wananchi wanatakiwa kufuata taratibu juu ya sheria za matumizi ya ardhi, ili kuondokana na migogoro inayohusiana na ardhi.

Akiwa katika ziara hiyo, mkuu huyo alisema ziara hiyo inalenga kujitambulisha na kutatua kero za wananchi, lakini kuangalia miradi ya wananchi ambayo inaendelea katika maeneo hayo.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi katika kata hiyo, Ogra Steven Mtundu, alisema kero inayowakabili ni ukosefu wa shule ya kata ambapo wanafunzi wamekuwa wakitembea umbali mrefu kwenda shule wanazopangiwa kusoma.

Alisema ni vyema suala la kuwa na shule ya kata karibu likapewa kipaumbele.

Aidha, alisema kuna tatizo la umeme jambo ambalo linakwamisha kuanzisha miradi mbalimbali ya ujasiriamali ili kujiongezea kipato.

**Maeneo ambayo watu walijimilikisha waondoke mara moja hivi tukitaka kuwekeza tutakwenda kuwekeza bila matatizo**

# Uzalishaji kahawa kupaa kwa tani 150,000

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imeanzisha mashamba makubwa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa nchini kutoka tani 50,000 hadi tani 200,000 kwa mwaka.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Mazao katika wizara hiyo, Nyasebwa Enock, alielezea jana wakati wa kikao cha wadau wa kahawa cha kujadili mpango mpya wa kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja yenye mashamba ya wakulima wadogo ndani yake.

Alisema mpango huo unalenga wakulima wadogo kuongeza tija na kuongeza uzalishaji huo huku lengo halisi likiwa ni kufikia tani 300,000 kwa mwaka kama ilivyopendekezwa katika ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025.

Alieleza kuwa mpango huo utawasaidia wakulima kupata huduma za ugani kwa urahisi kwa kuwa pamoja.

"Tumekuwa na uzalishaji mdogo kwa sababu ya utumiaji mdogo wa pembejeo za kilimo pamoja na miche bora, mbolea na viuatilifu. Tumegundua pia kutawanyika kwa wakulima kunachangia wao kutopata huduma za ugani, " alisema.

Enock alisema serikali inataka wakulima kutumia kikamilifu uwepo wa vyama vya ushirika ambavyo watavitumia kwa ajili ya kuagiza pembejeo za kilimo hasa mbolea na kuwauzia wanachama wake kwa bei ya chini.

Alisema vyama vya ushirika ni injini muhimu katika kukuza uzalishaji wa kahawa nchini na ndio maana serikali imekuwa ikivibana vyama vinavyofanya vibaya na hata kuvifuta.

Mkurugenzi huyo aliwataka wakulima hao kuhakikisha wanatumia teknolojia zilizopo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuongeza tija.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), Prof. Jamal Adam, alisema bodi hiyo ina matumaini kuwa hatua mpya zitakazochukuliwa zitaongeza uzalishaji.

Alisema upatikanaji wa pembejeo za kilimo na matumizi bora ya kanuni za kilimo kutaongeza uzalishaji mara mbili kwa kutumia miti iliyopo.

Alibainisha mwaka jana zao la kahawa lilichangia zaidi ya dola za Marekani milioni 200 katika mapato ya fedha za kigeni kwa serikali na linabaki kuwa moja ya mazao ya mkakati ya biashara nchini.

Kwa upande wake, mmoja wa washiriki kutoka Rafiki Coffee Limited, Rashid Mohammed alilalamikia wadau kwa kushindwa kutoa habari sahihi kwa wakulima na kusababisha wakulima wengi kuhamia kwenye mazao mengine ya biashara.

Aliiomba serikali kuimarisha mawasiliano ili kuwasaidia wananchi.



# Wakulima, wafugaji wafunzwa uandaaji bajeti mrengo kijinsia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wakulima na wafugaji wa Kijiji cha Shibolya kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameanza kunufaika na elimu ya upangaji bajeti yenye mrengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia ambayo imetolewa na Shirika lisilo la kiserikali la Elimisha.

Mmoja wa wafugaji waliopata elimu hiyo, Rehema Nsolo, alisema wanawake wamekosa kipaumbele cha kushirikishwa kwenye utoaji wa maamuzi, jambo linasababisha familia nyingi kutokuwa na bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Nsolo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika Kijiji cha Shilolya wakati Shirika la Elimisha likitoa elimu ya upangaji bajeti yenye mlengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia uliokuwa na lengo la kuweka usawa katika matumizi ya raslimali fedha.

**Upangaji huo wa bajeti utasaidia kufahamu unatumia shilingi ngapi kwa siku, shughuli unayoifanya ikuingizie shilingi ngapi ili uweze kukidhi mahitaji yako.**

Alisema wanawake wengi wanajukumu la kuhakikisha mazao na mifugo linakuwa salama, lakini unapofika muda wa mauzo wanaume ndiyo wanahusika na shughuli zote za uuzaji na kupanga matumizi ya fedha hizo bila kuwahusisha wake zao.

"Asilimia 80 ya wanawake vijijini ndiyo wazalishaji, lakini wengi hatuna maamuzi wakati wa mauzo ya tulichozalisha, elimu hii imetusaidia kutambua haki zetu hivyo ni wakati wetu kupigania bajeti yenye mlengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia," alisema Nsolo.

Aliwataka wanawake wote wanaojihusisha na kilimo pamoja na ufugaji kuhakikisha hawako nyuma unapofika wakati wa mavuno na upangaji wa bajeti kushiriki kama wazalishaji wakubwa badala ya kuwaachia wanaume ambao wakati mwingine fedha za mavuno huzitumia kuhonga michepuko na ulevi.

Akieleza lengo la utoaji wa elimu hiyo, Festo Sikagonamo, alisema upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia utasaidia kupunguza vichocheo vya umaskini kwenye jamii, wizi, rushwa, kuongeza ufanisi wa kazi na kuwafanya watu kuwa na matumizi yanayoendana na kipato.

Alisema upangaji huo wa bajeti utasaidia kufahamu unatumia shilingi ngapi kwa siku, shughuli unayoifanya ikuingizie shilingi ngapi ili uweze kukidhi mahitaji yako.

Alisema ili kuhakikisha familia na jamii kwa ujumla inaondokana na changamoto ya matumizi mabaya fedha kwa kutokufuata bajeti ya Shirika la Elimisha kwa kushirikiana na serikali linasaidia masuala ya kimkakati na linazingatia malengo na shabaha ya dira ya maendeleo ya Taifa ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.



Mgombea ubunge Jimbo la Mbeya Mjini, kupitia CHADEMA, Joseph Mbilinyi 'Sugu', akihutubia mkutano wa kampeni uliofanyika katika Uwanja wa Shule ya Msingi Nzovwe jijini Mbeya juzi. **PICHA: FRANCIS DANDE**

# 820 wanolewa uzalishaji wa vyakula

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA 825 kutoka Kata za Inyala, Itewe na Utengule Usongwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji wa vyakula vyenye virutubisho vya lishe kama vile mbogamboga na matunda kwenye skimu za umwagiliaji ili kuimarisha afya ya mama na mtoto.

Akizungumza na Nipashe juzi, Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Damas Massawe, alieleza kuwa lengo ya kutoa mafunzo hayo ni kuongeza uzalishaji wa virutubisho ambavyo vitasaidia kuondoa udumavu kwa watoto.

Massawe alisema Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika katika utekelezaji wa shughuli zake imesimamia uzalishaji wa vyakula vyenye virutubisho ili kuimarisha afya ya mama na mtoto.

Alieleza kuwa katika kuongeza uzalishaji idara hiyo ilitumia maofisa ugani kutoka ngazi za vijiji na kata kutoa elimu kwa kushirikiana na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kama vile Feed the Future.

"Tulibaini baadhi ya sababu ambazo zinachangia udumavu kwa watoto kuwa ni kukosa viini lishe kutoka kwenye matunda na mbogamboga hivyo idara ya kilimo katika kupunguza tatizo hilo tuliandaa mafunzo kwa wakulima kujua namna ya kuongeza virutubisho wa watoto hao," alisema Massawe.

Alisema katika kukabiliana na udumavu kwa watoto idara hiyo inakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa vitendea kazi kama vile pikipiki kwa maofisa kilimo kwenye kata na vijiji pamoja na ubovu wa gari la idara hali inayosababisha kutofanya kazi kwa ufanisi.

Alisema idara imejipanga kuongeza jitihada za kuwezesha uzalishaji wenye tija kwenye sekta ya mboga na matunda ikiwa ndio sekta yenye vyakula muhimu vya lishe kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta zisizo za kiserikali zilizopo ndani ya halmashauri hiyo.

Miongoni mwa wananchi hao, Mbukwa Mwasandube, kutoka Kata ya Ijombe, alieleza kuwa sababu iliyochangia udumavu kwa watoto ni mtindo wa maisha, alisema wazazi na walezi wako bize na shughuli za uzalishaji na ujasiriamali na kusahau wajibu wao kwa watoto.

Alisema ili kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto serikali kwa kushirikiana na taasisi nyingine zitoe elimu ya umuhimu wa malezi kwa watoto hasa kwenye lishe.

"Serikali kupitia idara mbalimbali imejitahidi kutoa elimu ya wazazi na walezi kuzingatia milo kamili na kuzalisha vyakula vyenye virutubisho, lakini wamesahau elimu ya malezi kwa watoto," alisema Mwasandube.

# Mkakati wa kuongeza uzalishaji maharage waja

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KIKUNDI cha wanawake wanaolima maharage, Kata ya Mshewe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kijulikanacho 'Zinduka', kimesema kwa sasa kinakusudia kuongeza uzalishaji wa zao hilo baada ya kupewa mtambo wa kisasa wa kukaushia zao hilo.

Kikundi hicho kilikabidhiwa mtambo wa kisasa wa kukaushia zao hilo unaotumia nishati ya jua (Bean Solar Drier) na Taasisi ya Kimataifa inayoshughulikia kilimo cha mazao ya Kitropiko (Ciat) ili kukisaidia kikundi hicho kuokoa mazao yaliyokuwa yanaoza kutokana na kushindwa kukauka hasa kipindi cha mvua.

Wakizungumza na Nipashe wanachama wa kikundi hicho walisema kabla ya kupewa mtambo huo walikuwa wanapata shida kukausha maharage kipindi cha mvua na kusababisha sehemu kubwa ya mavuno kupotea kwa kuoza.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Witness Sikayange, alisema kikundi hicho kina wanachama 21 na kinalima ekari 300 za maharage na kwamba kwa mwaka wanalima misimu mitatu ukiwamo mmoja wa kiangazi ambao wanatumia mbinu ya umwagiliaji.

Alisema mavuno mengi wanavuna msimu wa mvua na hivyo kusababisha mazao kuoza yakiwa shambani ama yakiwa yamevunwa na kuhifadhiwa ndani ya nyumba na hivyo kukosa soko hali ambayo imekuwa ikiwasababishia hasara.

Alisema kikundi hicho kimekuwa kikishirikiana na wataalamu wa kilimo kutoka katika taasisi mbalimbali za serikali na binafsi ikiwamo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole, wataalamu kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya pamoja na ofisa kilimo wa kata hiyo.

Alisema awali kabla hawajaanza kushirikiana na wataalamu hao walikuwa wanatumia mbegu za kienyeji pamoja na mbinu duni za kilimo hali iliyokuwa inawafanya wazalishe chini ya kiwango lakini kwa sasa wanazalisha kuanzia kilo 600 mpaka 800 kwa ekari.

Mratibu wa Mtandao wa Utafiti wa Maharage Kusini mwa Bara la Afrika, Rolland Chirwa, alisema mtambo huo una uwezo wa kukausha tani moja ya maharage kwa siku na kwamba ni salama kwa mazao kutokana na kuzuia mifugo kula na mvua kunyeshea.

Alisema waliamua kukisaidia kikundi hicho cha Zinduka baada ya kubaini kuwa kina uwezo mzuri wa kuzalisha na kina watu wanaojituma ikilinganishwa na vikundi vingine.



# Mgombea urais AAFP apigia debe CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha Wakulima (AAFP) ambaye ni mgombea urais wa Zanzibar kupitia chama hicho, Said Soud Said, amesema vyama vya upinzani haviwezi kushinda uchaguzi kutokana na baadhi ya viongozi wake kugubikwa na ubinafsi, choyo na ulafi wa madaraka.

Alisema baadhi ya viongozi wa vyama hivyo wameweka mbele ulafi wa madaraka kwa maslahi yao na sio kwa ajili ya wapigakura wao na ndio wamekuwa wakitoka chama kimoja kwenda kingine kwa kutafuta nafasi ya kuwa viongozi wakuu.

Mgombea huyo alisema hayo kisiwani Pemba, wakati alipokuwa akizungumza na mwandishi wa habari kufuatia migangano ya kimaslahi kwa viongozi wa vyama vya upinzania.

Alidai kuwa chama pekee ambacho kimekuwa kikishinda katika chaguzi zilizopita na zinazokuja ni Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokana na kujipanga kwake kimkakati na kutokana na kura zake inazopewa na wapigakura kwa vile hazigawanyiki.

**Kura za Chama Cha Mapinduzi, hazigawanyiki tafauti na vyama vya upinzani, hivyo kuungwa mkono na wapigakura wao waliowengi imekifanya chama hicho kuendelea kushinda katika changuzi mbalimbali.**

"Kura za Chama Cha Mapinduzi, hazigawanyiki tafauti na vyama vya upinzani, hivyo kuungwa mkono na wapigakura wao waliowengi imekifanya chama hicho kuendelea kushinda katika changuzi mbalimbali," alisema.

Alieleza chama hicho kikongwe katika siasa za Tanzania na barani Afrika kimekuwa na mipango imara hata wanaposimamisha wagombea wake, hakikurupuki na yule anayesimama kwenye kura za maoni hata kama kura zake hazikutosha huridhika na kumuunga mkono mwenzake aliyepata kura za kutosha.

Soud ambaye ni waziri katika serikali ya umoja wa kitaifa, alisema ni tofauti na baadhi ya viongozi wa vyama upinzani kama mtu hakupata yeye anahama chama na kujiunga na chama kingine bila ya kukifanya utafiti ilimradi apate nafasi anayohitaji kwa maslahi yake binafsi.

"Sisi viongozi wa vyama vya upinzani, iwapo tunataka kushinda katika chaguzi za vyama vingi zinazokuja, ni lazima tusome mipango ya Chama Cha Mapinduzi, na turidhike na maamuzi ya vyama vyetu na sio kuweka mbele ubinafsi na ulafi wa madaraka vinginevyo tutaendelea kuongozwa na chama hicho kila mara," alidai Soud.

Aliendelea kudai kuwa viongozi wa vyama vya upinzani wataendelea kulalamika pale wanaposhindwa kwa sababu bado hawajaona wanapokosea kwenye chaguzi mbalimbali na kila mmoja analazimisha awe kiongozi wa ngazi ya juu japo wananchi wameshachoka nae.

Akizungumzia kiongozi anayehitajika kwa sasa alieleza nafasi ya urais kwa Zanzibar ni yule ambaye ana uwezo wa kuwahudumia wananchi.

Aliwataka wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla wawaunge mkono viongozi wenye uwezo wa kuwaletea maendeleo na waangalie na wawapime na uongozi wao uliopita.

Soud alisema sio vyema kuchagua kwa kubahatisha kwa mtu ambaye hajawahi kuwaletea maendeleo na ni jambo la busara kuchagua viongozi wa vitendo na sio maneno.




Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Mahmod Thabit Kombo (kulia), akimtambulisha Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (wa pili kulia) kwa Balozi Mdogo wa Italia, Stefano Totisco (kushoto), wakati wa mchaparo ulioandaliwa na benki hiyo, kwa wafanyabiashara wa Zanzibar juzi. Wa (pili kushoto) ni Meneja wa Kadi na Biashara wa benki hiyo, Philbert Casmir. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanawake walioko kwenye ndoa wapewa changamoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Jaji Mshibe Ali Bakari, amewataka wanawake wa Zanzibar waliomo katika ndoa kuacha kuwapa fedha waume zao wanapotaka kununua vitu vya thamani, badala yake wende wakanunue wenyewe.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, alisema kuwa wanawake wengi waliomo katika ndoa hudhulumiwa hasa pale ndoa inapovunjika kwa sababu wanaponunua vitu vya thamani huwakabidhi fedha waume zao, hivyo wanaume hujifanya mali hizo ni zao.

"Unapompa mume fedha akanunue gari, kiwanja au nyumba hujifanya mali hizo ni zao wanaume kwa sababu risiti au nyaraka hujiandika majina yao wanaume wakati fedha sio zao," alisema Jaji Mshibe.

Alieleza kuwa wanawake wengi wa Zanzibar hudhulumiwa na hukosa haki zao kwa sababu hawana vielelezo vyovyote kuwa mali wanazomiliki ni zao na ndipo kesi hizo zinapofikishwa mahakamani wanaume hushinda hata kama mali sio zao, lakini huwa na vielelezo.

Jaji huyo aliwataka wanawake kuhakikisha wanaponunua vitu vya thamani kuwa na vielelezo ili inapotokea migogoro katika ndoa mali hizo zibaki kuwa zao.

Akizungumzia kuhusu vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto, alisema bado jamii haijawa tayari kutokomeza vitendo hivyo na ndio maana vimekuwa vikiendelea kuwapo.

Alieleza kuwa wananchi wengi wamekuwa wakilitupia lawama Jeshi la Polisi, Mahakama na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuhusu vitendo hivyo wakidhani kuwa taasisi hizo ndizo zinazokwamisha kesi hizo, lakini tatizo lipo kwa jamii na wala sio vyombo hivyo.

Alisema jamii isiridhike kumtia hatiani mtuhumiwa aliyefanya vitendo vya udhalilishaji kwa sababu hata mtuhumiwa akifungwa mtoto kishaharibiwa, hivyo ni vyema kuzuia vitendo hivyo visitokee kabisa.

Aidha, aliitaka jamii kubadilika katika malezi na kuwa na malezi ya pamoja ili kumlinda mtoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji na kuachana na muhali mtoto anapodhalilishwa.

Akisoma risala kwa niaba ya watoto wenzake Salumu Mohammed kutoka Shule ya Tumekuja, alisema watoto wa kike wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo mimba na ndoa za mapema.

# Jamii yashauriwa vijana walioacha dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Kinga, Tiba na Marekebisho ya Tabia kutoka Tume ya Kuratibu na Kuthibiti Dawa za Kulevya Zanzibar, Said Ramadhan Maulid, amesema ushiriki wa vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya katika kusaidia jamii ni sehemu ya kufuta makosa walipotumbukia katika janga hilo.

Alisema wamekuwa na utaratibu maalumu wa vijana waliopata nafuu kutoka nyumba za kurekebisha tabia (Sobber House) kushiriki katika kazi za kijamii ikiwamo kusafisha mazingira kwa wazee pamoja na kuwavusha njia watoto na watu wenye mahitaji maluum.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Upataji Nafuu katika nyumba za wazee Sebleni Mjini Zanzibar, Maulid alisema vijana hao wamekuwa na mwamko wa kutambua umuhimu kutunza afya zao na kushiriki katika shughuli tofauti za kijamii.

"Tumekuwa na utaratibu kama huu kila mwaka tunapoazimisha wiki ya upataji nafuu kwa vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya kwa kushiriki katika kazi za kijamii na vijana wetu wamekuwa wakionyesha mwitikio mkubwa wa kufanya kazi hizi ikiwa ni ishara ya kuomba msamaha kwa jamii kwa vitendo walivyokuwa wakivifanya wakati wakitumia dawa," alisema Maulid.

Aidha, alisema shughuli hiyo ya usafi imefanywa na vijana kutoka nyumba mbalimbali za kurekebisha tabia za Unguja, na kwamba amaridhishwa na hamasa inayoonyeshwa na vijana hao katika kujitolea kwenye shughuli za kijamii.

Naye Meneja wa Sober House ya Bububu, Mansoor Haji Suleiman, pamoja na mkuu wa kituo cha kulelea watoto yatima Mazizini, Pili Sadalla Mussa, walieleza kuridhishwa na ushiriki wa vijana hao katika kazi za kusaidia jamii na kunawajengea heshima na uaminifu.

Waliitaka jamii kuacha kuwanyanyapaa vijana walioacha dawa za kulevya na badala yake kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za kijamii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**DEREVA NA MAUZO**, KATIKA KAMPUNI YA MAJI NAFASI 8 0767 - 269677.

NIPASHE NI JIBU LAKO

Nipashe

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

Nipashe

## KUPOTEA KWA CHETI



**NAOMI BURTON PANJA** anatangaza kupotelewa kwa vyeti viwili cha FORM FOUR index namba **S. 2925-0089** kilichotolewa na shule ya secondary ya **NALYELYE MBOZI SONGWE 2016** , NA CHA CHUO index namba **CGA/2017/07/2121** kilichotolewa na chuo cha MATI MTWARA 2019, POLISI TAARIFA ; **MTW/MTW/RB/476419/2020.**

115940102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURIN MDAIWA**
**(MCA/84)**

**Mahakama ya mwanzo ya KYELA MJINI**
**Wilaya ya KYELA**

**MADAI NAMBARI 88 YA 2020**

**Mdai MANYANYA OIL LTD**

**Mdaiwa EAFCO (VEDASTUS MATHAYO)**

**Kwakua mdai/wadai ameleta madai yake MADAI YA PESA 7,276,440/=**

Kwahiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya JUMATATU Tarehe **26/10/2020 saa 2.30** asubuhi,kwa kujibu madai hayo nisiku ya kukatwa shauri lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuudhuria siku iliyotajwa apo juu ,mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa . Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 9/10/2020.

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA KYELA KYELA MJINI

115940702

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**TITO GEORGE KONZO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 330 BKM** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi. **MBE/MBE/RB/730583/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KABOYA JUMA WENGE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA **KADI YA PIKIPIKI** YENYE **NAMBA ZA USAJILI MC 362 CHQ AINA YA SUNLG.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KA H/TR/RB/345/2020.**

21593982

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII www.ippmedia.com

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Nigeria yavunja kikosi maalum cha polisi

**LAGOS, Nigeria**

BAADA ya wiki moja ya maandamano nchini Nigeria, ofisi ya rais imeidhinisha kuvunjwa kwa Kikosi Maalum cha Polisi (SARS), kinachotuhumiwa kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Kabla ya hatua hiyo, vijana wa Nigeria waliendelea na maandamano yao mwishoni mwa wiki, kupinga kikosi hicho.

Kabla ya maandamano hayo, wito mbalimbali ulitolewa kwenye mitandao ya kijamii na wanaharakati mbalimbali husani vijana.

Tangu awali, maandamano hayo yaliungwa mkono na nyota za mitindo ya Afropop, ambao walipaza sauti na kuitaka jumuiya ya kimataifa kuingilia kati.

Wanamuziki kama vile Davido au Wizkid wamekuwa wakituma taarifa mbalimbali kuhusiana na kikosi hicho cha polisi, wakiomba kivunjwe mara moja.


Wizkid alijiunga na kundi la raia wa Nigeria katika maandamano yaliyofanyika Jumapili hii, Oktoba 11 jijini London, Uingereza.

Mkuu wa Polisi alitangaza kuvunjwa kwa kikosi cha kupambana na ujambazi, kulingana na matakwa ya waandamanaji.

Wakati huo huo, mkuu wa polisi aliahidi kuundwa kwa tume ya uchunguzi, ili kuchunguza uhalifu uliofanywa na polisi dhidi ya raia, ambao mashirika ya kiraia yatashirikishwa.

Nigeria imevunjilia mbali kikosi chake maalum cha polisi, baada ya maandamano ya umma kutokana na madai ya ukatili wa polisi.

*RFI*



Ruto (kushoto) na Kenyatta katika tukio linaloonyesha kuwa wawili hao wana tofauti za kisiasa. **PICHA: MTANDAO.**

# Afya ya Trump yaendelea vizuri

**WASHINGTON, Marekani**

ZAIDI ya wiki moja baada ya kuambukizwa virusi vya corona, Rais wa Marekani, Donald Trump, amesema anajisikia yuko vizuri sana, na hatumii dawa yoyote.

Katika mahojiano kwa njia ya simu na televisheni ya Fox news, Trump, alisema, "nimevishinda virusi hivi vibaya vya China, ni kama nina kinga ya mwili labda kwa muda mrefu, muda mfupi, labda maisha yangu yote."

Katika mahojiano hayo, mwanahabari hakumuuliza iwapo vipimo vilionyesha kwamba hana tena virusi vya corona, ambavyo vimeshaua zaidi ya watu 200,000 na kuambukiza zaidi ya milioni saba nchini Marekani.

Muda mfupi baada ya kufanya mahojiano na televisheni ya Fox, Trump aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter, kwamba madaktari wake wamethibitisha kuwa amepona kabisa na kwamba hivi sasa hawezi kuambukizwa corona, wala hawezi kuwaambukiza watu wengine.

Baadaye kampuni ya Twitter ilisema "ujumbe wa Trump unakiuka maadili ya mtandao wa Twitter kuhusu kusambaza habari za uongo na kupotosha za janga la Covid-19.

# Mvutano Kenyatta, Ruto washika kasi

**NAIROBI, Kenya**

MVUTANO bado unaendelea kuripotiwa kati ya Rais Uhuru Kenyatta na Makamu wake, William Ruto.

Mvutano huo unahusiana na uchaguzi ujao wa urais, mwaka 2022.

Ingawa kampeni bado haijaanza, wafuasi wa kambi zote mbili tayari wamekuwa wanaendelea kukabiliana, bila huruma kwa miezi kadhaa.

Mkutano wa Makamu wa Rais William Ruto, ulipigwa marufuku na mamlaka, ikibaini kwamba ni katika hali ya kuimarisha usalama wa nchi.

Uamuzi ambao umesababisha ukoo wa Ruto kupandwa na hasira.

Sintofahamu inaendelea kuripotiwa katika ngazi za juu ya serikali, nchini Kenya kwa miezi kadhaa.

Rais Kenyatta ataondoka madarakani mwaka 2022. Alitarajiwa kumuunga mkono makamu wake wa Williamo Ruto kulingana na mkataba walioafikiana.

Lakini Uhuru Kenyatta, inadaiwa kuwa ameanza kumtafuta mrithi wake mwingine.

Tangu wakati huo, Ruto amejitenga. Miaka 2 kabla ya uchaguzi, tayari ameanza kuhamasisha kambi yake na kutoa jumbe za uhasama dhidi ya ukoo wa Kenyatta. Matokeo:

Kambi hizo mbili zimekuwa zikishambuliana, hadi kusababisha vifo. Siku chache zilizopita, maandamano ya kisiasa yaligeuka kuwa machafuko na kusababisha vifo vya watu wasiopungua 2.

Viongozi wa nchi hiyo wana wasiwasi: "Ikiwa hakuna kinachofanyika kwa sasa kutuliza hali ya mambo, Kenya inaweza kuingia kwenye machafuko." Hali inayofanana na ile ya mwaka 2007, wakati vurugu za baada ya uchaguzi zilisababisha vifo vya watu zaidi ya elfu moja.

RFI

# Kombora jipya la Korea laipa Marekani tumbo joto

**PYONGYAQNG, Korea Kaskazini**

KOREA Kaskazini imezindua kombora jipya la masafa marefu (ICBM), ambalo ukubwa wake umeshangaza wachambuzi wa masuala ya silaha ya nchi hiyo.

Mtaalamu wa masuala ya ulinzi, Melissa Hanham anaelezea kombora hilo ni tishio kwa Marekani na ulimwengu.

Katika kuadhimisha miaka 75 ya chama tawala cha Workers Party cha nchi hiyo, imefanya gwaride la kijeshi mwishoni mwa wiki.

Hafla hiyo iliyoangaziwa sana, ilionyesha fahari yake na hali zote, ambazo ulimwengu umetarajia kutoka kwa maonyesho ya watu wa Korea Kaskazini.

Pia tukio hilo liliandamana na hotuba yenye hisia kutoka kwa mwenyekiti wa chama hicho Kim Jong-un, ambaye ni rais wa nchi hiyo, alidondosha machozi akielezea magumu, ambayo Korea Kaskazini imeyapitia.

Januari Mosi, mwaka huu, Rais Kim alitoa hotuba yake ya mwaka mpya, ambapo alitangaza kuwa Korea Kaskazini "inatengeneza mfumo wa kisasa wa silaha, ambazo humilikiwa na nchi zilizoendelea pekee". Alielezea kuwa ni zoezi la kimkakati akimaanisha mfumo wa silaha za nyuklia.

Kim akiigusia Marekani, alisema "katika siku za usoni, kadiri Marekani inavyokaa kwa muda na kusita katika usuluhishi wa uhusiano wa DPRK na Marekani ndivyo itakavyoshindwa zaidi mbele ya nguvu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea, ambayo inaendelea kuimarika na nguvu zaidi ilivyotabiriwa.

ICBM mpya ni silaha ya mkakati iliyoahidiwa na Bwana Kim. Inalenga Marekani kabisa, na imekuwa kama jambo lililofanyiwa maamuzi mbele ya mazungumzo yaliyoshindwa na serikali ya Trump.

Mwaka 2010, Korea Kaskazini ilinunua magari matano makubwa kutoka China na kuyabadilisha kuwa na uwezo wa kurusha makombora TELs.

Korea Kaskazini, imeunda sekta yake ya viwanda kuweza kufanyia mabadiliko mbali na kuzalisha mitambo yake ya kurusha makombora.

*BBC*




# PSG BADO YAKOMAA NA SAINI YA RONALDO

**PARIS, Ufaransa**

CRISTIANO Ronaldo ameripotiwa kuwa ni chaguo namba moja kwa Paris Saint-Germain, katika usajili ujao wa kipindi cha majira ya joto.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 35, yupo kwenye msimu wake wa tatu pale Juventus baada ya mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or kufurahia maisha kule Real Madrid na Manchester United.

Lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwa klabu hiyo kutoka kule Turin na uvumi, bado unaendelea.

PSG inaweza kumsajili Ronaldo kwa mara nyingine tena, kwa mujibu wa gazeti la CalcioMercato.

Hata hivyo, ripoti hiyo inasema Ronaldo anataka kuendelea kutumikia mkataba wake pale Juventus, ambao unamalizika mwaka 2022.

Ronaldo tayari ameifungia mabao matatu Juventus katika mechi mbili za Ligi Kuu ya Italia, Serie A msimu huu.

# SOUTHGATE

## NA MATUMAINI MAPYA KIKOSI CHA ENGLAND

**LONDON, England**

GARETH Southgate bado anaona kuna nafasi ya kuimarika kwa England, baada ya kuibuka na ushindi, dhidi ya Ubelgiji kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA na kusema ni wakati "mkubwa" kwa wachezaji wake.

Mason Mount aliiwezesha England kupata ushindi wa mabao 2-1, pale kwenye dimba la Wembley dhidi ya mpinzani huyo, ambaye awali hakuwahi kufungwa tangu Novemba 2018.

Timu hizo mbili zilipata penalti kipindi cha kwanza, huku Ubelgiji wakianza kuwa mbele na baadaye England kusawazisha na kupata ushindi wake wa 20 katika mechi 21 zilizopita.

Baada ya mchezo huo, Southgate alionyesha kufurahia kiwango cha wachezaji wake kwenye mchezo huo.



"Wachezaji walikuwa kwenye kiwango cha kuvutia na walionyesha kwamba wanahitaji ushindi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulijua ubora wa wapinzani wetu na walikuwa na kiwango cha juu, lakini sisi tulicheza vizuri zaidi na kuweza kupata ushindi.

"Pamoja na yote, naona kuna nafasi ya timu kuimarika zaidi na nina imani kubwa kwenye mchezo ujao mambo yatakuwa bora zaidi."




# AOUAR ATOA SABABU KUTOJIUNGA ARSENAL

**LYON, England**

HOUSSEN Aouar amezungumzia namna anavyoona ufahari kuichezea Lyon, baada ya Arsenal kushindwa kumsajili wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto.

'Washikabunduki' hao walikuwa wakihuishwa na kutaka kumsajili kiungo huyo wa Ufaransa, Aouar lakini dili lilishindikana na wakafanikiwa kuinasa saini ya Thomas Partey kutoka Atletico Madrid.

Wakati mchezaji mwenzake, Memphis Depay ameonyesha kuhuzunika kwake kwa kutokamilika kwa uhamisho kwenda Barcelona, Aouar amesisitiza ana furaha kubakia hapo Lyon.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, pia alikuwa akihusishwa na kuwaniwa na miamba wa LaLiga, Real Madrid, wakati mkataba wake ukiwa unamalizika mwaka 2023.

"Haikuwa muhimu kwenda Arsenal au sehemu yoyote, najisikia fahari kubaki hapa Lyon," alisema Aouar akiiambia Telefoot.

"Kwa kawaida unatakiwa uwe na chaguo na nikaamua kubaki hapa na ninafuraha kubwa kuwapo Lyon.

"Hili ni jiji langu nililokulia, na hii ni klabu yangu, hivyo lilikuwa jambo bora kwa mimi kubaki hapa."

## HABARI MICHEZO



# WENGER

## ASHANGAA OZIL KUKOSA NAFASI ARSENAL

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, ameonyesha kushangazwa kwa Mesut Ozil, kukosa nafasi kwenye klabu hiyo.

Ozil wiki iliyopita aliachwa kwenye orodha ya wachezaji 24 watakaoshiriki michuano ya Ligi ya Europa kwenye hatua ya makundi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, bado hajapata nafasi kwenye kikosi cha Mikel Arteta msimu huu na mara ya mwisho kucheza ilikuwa Machi mwaka huu kabla ya mlipuko wa virusi vya corona.

Uhamisho wa kwenda popote ulishindikana kutokana na mshahara wake, ambapo analipwa kiasi cha pauni 350,000, kwa wiki.

Wenger ndiye aliyemnunua mshindi huyo wa Kombe la Dunia kutoka Real Madrid mwaka 2013 na sasa anashangazwa na kushindwa kupata nafasi, kwenye kikosi hicho.

"Alipotea kwenye rada wakati nilipoondoka klabuni pale," alisema Wenger akiiambia Welt am Sonntag.

"Ni mchezaji wa kiwango cha juu, sijui kwa nini kwa sasa hana nafasi. Pengine soka la kisasa halihitaji aina yake ya uchezaji."

## DEPAY AWAZA BARCA JANUARI

**LYON, England**

MEMPHIS Depay anatarajia kuna klabu zitamhitaji zaidi Januari, baada ya uhamisho wake wa kwenda Barcelona kushindikana wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Straika huyo wa Lyon alionekana kama anakwenda kujiunga na kocha wake wa zamani wa timu ya Taifa ya Uholanzi, Ronald Koeman kule 'Blaugrana' na tayari makubaliano binafsi yalishafanyika.

Hata hivyo, dili hilo lilishindikana, huku Depay akikiri kwamba "sheria kadhaa" zilimzuia yeye kujiunga na Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, na anaamini kwamba wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari anaweza kupata nafasi ya kujiunga na timu nyingine.

"Nina umri wa miaka 26, na uhamisho wangu hautagharimu chochote," alisema akiiambia BN DeStem.

"Hivyo, tunaweza kutarajia klabu kuonyesha nia kwangu.

"Pengine itakuwa haraka Januari. Tutaaangalia namna mambo yanavyokwenda."




## ROBINHO ARUDI TENA SANTOS MARA YA NNE

**SAO PAULO, Brazil**

NYOTA wa Brazil, Robinho amerudi katika klabu ya Santos kwa mara ya nne baada ya kusaini mkataba wa muda mfupi na klabu yake hiyo ya utotoni.

Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City na Real Madrid, ameingia mkataba wa kuichezea klabu hiyo hadi mwishoni mwa msimu huu.

Robinho amekuwa hana timu tangu alipoondoka katika klabu ya nchini Uturuki ya Istanbul Basaksehir, Agosti mwaka huu na nyota huyo mwenye umri wa miaka 36, alionyesha furaha yake kurudi katika klabu yake hiyo.

"Hapa mara zote ni nyumbani kwangu," alisema baada ya kusaini Santos, ambao kwa sasa wanashika nafasi ya saba kwenye msimamo baada ya mechi 14.

"Kazi yangu ni kuisaidia timu uwanjani na kuifanya Santos kuwa na mafanikio makubwa kadri inavyowezekana."

Robinho alianza kucheza soka hapo Santos kabla ya kuhamia Ulaya, awali akijiunga na Real Madrid, kabla ya kusajiliwa na Manchester City mwaka 2008.

Mara mbili alirudi Santos kwa mkopo mwaka 2010 na 2014, baada ya kukaa misimu minne na AC Milan.

Pia, alicheza soka nchini China kabla ya kwenda Uturuki na aliichezea Atletico Mineiro mwaka 2016 na 2017.

Robinho, ambaye alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu akiwa na Santos, alicheza mechi 100 kwa Brazil kati ya mwaka 2003 na 2017, akifunga mabao 28.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RAIS AKATAA MESSI NI MBELEKO YA LALIGA

Pengine kama mchezaji, lakini kwa yeye kwenye biashara ya soka, kwa sababu ni mashine...

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas, amepuuzia athari za nyota wa Barcelona, Lionel Messi kama angeihama klabu yake hiyo.

Messi aliwasilisha maombi ya kutaka kuondoka baada ya msimu mbaya wa 2019-20, ambao ulishuhudiwa Barca wakinyanyaswa kwa kufungwa mabao 8-2 na Bayern Munich kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pia walipokonywa taji la Ligi Kuu ya Hispania na Real Madrid, na baadaye mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or akaamua kubaki pale Camp Nou kwa msimu huu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, alikuwa na kipengele kwenye mkataba wake, ambacho kinamtaka kuondoka kwa euro milioni 700 na alikuwa akiwaniwa zaidi na miamba wa Ligi Kuu ya England, Manchester City, huku Paris Saint-Germain, Juventus na Inter pia zikimwania.

Alipoulizwa kuhusu Messi, Tebas aliwaambia waandishi wa habari: "Kama ambavyo mara zote nimesema, mara zote ningependa kumwona Messi kwenye LaLiga.

"Kama atabaki Barcelona, ni bora zaidi kwa Barcelona.

"Muunganiko wa Barcelona FC na Messi ni mzuri kwa Barca, kwa Messi na kwa LaLiga. Sina uhakika kama kuondoka kwake Barcelona, lingekuwa wazo zuri kwa Messi.

"Pengine kama mchezaji, lakini kwa Messi kwenye biashara ya soka, kwa sababu Messi ni mashine inayotengeneza kiwanda. Sidhani kama ingemsaidia yeye.

"Messi amebaki, lakini lazima nisema kwamba tayari tulishauza haki zote za TV za LaLiga kwa kipindi cha miaka minne ijayo na hakuna, ambaye alitupigia kutuambia wanasitisha makubaliano kama Messi angeondoka. Hakuna."

## KWA UFUPI

**CONTE AMTAKA AGUERO**

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte ana mpango wa kuwasilisha ombi la kumsajili mshambuliaji wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero, mwenye umri wa miaka 32, ambaye mkataba wake unatarajia kukamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Calciomercato)***

**WEST HAM YAGOMEWA KING**

OMBI la West Ham la kumnunua mshambuliaji wa Norway, Joshua King mwenye umri wa miaka 28, lilikataliwa na Bournemouth. ***(Mail)***

**POCHETTINO AAMULIWA UNITED**

MAOFISA wa Klabu ya Manchester United bado wanaelezwa kuwa katika mawasiliano na aliyekuwa Kocha wa Tottenham Hotspurs, Mauricio Pochettino iwapo watamfuta kazi, Ole Gunnar Solskjaer. ***(Star)***

**BENRAHMA ANG'ANG'ANIWA**

KLABU ya West Ham bado inaendelea na mazungumzo kuhusu usajili wa winga wa Brentford na Algeria, Said Benrahma mwenye umri wa miaka 25. ***(Evening Standard)***

**DEPAY KUONDOKA LYON**

ALIYEKUWA winga wa Manchester United, Memphis Depay, hajapuuza uhamisho wa kuelekea Barcelona Januari mwakani. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Uholanzi, alisalia na klabu ya Lyon, ili kumaliza mwaka wake wa mwisho baada ya klabu hiyo ya Catalunya kuwasilisha ombi msimu uliopita. ***(Marca)***

**PELLISTRI KURUDI URUGUAY**

NYOTA mpya wa United na Uruguay, Facundo Pellistri, mwenye umri wa miaka 18, tayari anapanga kurudi nyumbani kwao kuichezea klabu ya Penarol. ***(Sun)***

**GRACIA KWENDA BARCA**

KLABU ya Manchester City iliamua kumzuia beki wa Hispania, Eric Garcia, kwa msimu mmoja kwa sababu alikuwa na thamani kubwa kwao zaidi ya ofa ya Barcelona ya pauni milioni 18, kulingana na ofisa wa operesheni Omar Berrada. Garcia mwenye umri wa miaka 19, anaweza kuhamia kule Nou Camp kwa uhamisho huru msimu ujao baada ya kukataa kuongeza mkataba. ***(Manchester Evening News)***

**KOEMAN AMFUNGUKIA SUAREZ**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, amesema mshambuliaji wa Uruguay, Luis Suarez, mwenye umri wa miaka 33, angesalia katika uwanja huo, ili kuthibitisha umuhimu wake badala ya kuhamia Atletico Madrid. ***(Goal)***

**CORONA YAITIA NJAA BARCA**

BARCELONA imepoteza zaidi ya pauni milioni 181 kama mapato kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. ***(Telegraph)***

**BRIGHTON KUTOACHA MASHABIKI**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Brighton, Paul Barber, amewaambia wamiliki wa tiketi za mechi za Ligi Kuu ya England kwamba, hawataachwa nje iwapo watanunua tiketi za kila mechi zinazoonyeshwa. ***(Argus)***

**HAALAND CHUPUCHUPU UNITED**

KLABU ya Manchester United wangemsainisha mkataba mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland, kutoka klabu ya Red Bull Salzburg Januari, lakini kikwazo kilikuwa ni fedha iliyokuwa inatakiwa na wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa 20, ambaye alijiunga na Borrussia Dortmund. ***(ESPN)***

**STONES AIANIKA MAN CITY**

MLINZI wa Manchester City na England, John Stones mwenye umri wa miaka 26, alikataa kuondoka kwa mkopo kuelekea Totenham, kwa sababu hakutaka kuiondoa familia yake. ***(Star)***

# MWADUI YAPANIA KUWA YA KWANZA KUITOBOA AZAM FC

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mwadui FC, Adam Khalid, amesema kikosi chake kipo tayari kuhakikisha kinawasimamisha wapinzani wao, Azam FC katika mechi yao itakayopigwa Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam keshokutwa, Alhamisi.

Azam FC ndio wanaoongoza msimamo wa Ligi Kuu baada ya kuzoa pointi zote 15 katika mechi zao tano ilizocheza hadi sasa, huku Mwadui FC ikishika nafasi ya nane ikiwa na alama sita kutokana na kushinda mechi mbili na kupoteza tatu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Khalid alisema mpango wao ni mmoja tu, ambao ni kupata pointi tatu kwa kuwafunga Azam na kuwa wa kwanza kuwasimamisha katika kasi yao ya kupata matokeo mazuri kwenye mchezo huo wa raundi ya sita ya ligi hiyo.

Alisema kucheza usiku haitaathiri mipango hiyo kwa sababu tayari wamefanikiwa kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Yanga na wachezaji wake kucheza vizuri.

"Malengo yetu tuliyokuja nayo ni kupata pointi tatu, tukikosa hizo basi hata moja, suala la kucheza usiku kwangu halina shida, kikubwa tunaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri," alisema Khalid ambaye mchezo uliopita alifanikiwa kukiongoza kikosi chake kuzoa pointi zote tatu ugenini dhidi ya Namungo FC ya Mtwara baada ya kuichapa bao 1-0.

Kuhusu kazi ya Azam FC, kocha huyo alisema hana hofu juu katika hilo na hasa mfululizo wa 'Wanalambalamba' hao kutumia vema uwanja wao wa nyumbani na ugenini kupata matokeo.

"Ninawaheshimu Azam, ipo vizuri ila nimejipanga kuhakikisha tunakuwa timu ya kwanza kuwasimamisha wapinzani wetu hao katika uwanja wao wa nyumbani," alisema kocha huyo.

Katika mechi iliyopita, Azam FC iliibuka na ushindi wa mabao 4-2 nyumbani dhidi ya Kagera Sugar, huo ukiwa mchezo wao wa kwanza kuruhusu nyavu zao kutingishwa tangu msimu mpya wa ligi hiyo umeanza.

MATEMBEZI...




Baadhi ya Wafanyakazi wa EATV na East Africa Radio, wakiongoza matembezi maalumu ya kuchangia taulo za kike ('pedi') kwa shule mbalimbali za msingi na sekondari za Wilaya ya Kisarawe, matembezi hayo yalihitimishwa kwa hafla fupi iliyofanyika Shule ya Sekondari Minaki iliyopo wilayani humo na kupokelewa na Mkuu wa wilaya hiyo, Jokate Mwegelo juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Atlas Marathon sasa Oktoba 18

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Wakurugenzi na Uongozi wa Shule za Msingi na Sekondari za Atlas zilizopo jijini Dar es Salaam, umesema mbio za nusu fainali za Atlas Marathon zilizokuwa zifanyike siku ya kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, sasa zitafanyika Jumapili ya Oktoba 18, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na bodi hiyo jana, imeomba radhi wazazi, washiriki wa mbio hizo, wahitimu wa kidato cha nne na wale wa darasa la saba ambao sherehe zao za mahafali nazo pia sasa zitafanyika siku hiyo ya Oktoba 18.

"Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza na tuendelee na maandalizi ili Oktoba 18 ikifika tukimbie kizalendo kama ambavyo kauli mbiu ya mbio zetu inavyosema kwa lengo la kumuenzi Baba wa Taifa letu," alisema Mkurugenzi wa Shule za Atlas, Sylivanus Rugambwa.

Akizungumzia sababu ya kusogezwa mbele kwa matukio hayo mawili muhimu kwa shule hiyo, Rugambwa alisema ni kuwapo kwa ziara ya mikutano ya hadhara ya Rais John Pombe Magufuli katika Wilaya ya Kinondoni, hivyo bodi kuona kuwa si heshima kuwa na matukio mengine yanayovuta hadhira ya watu katika eneo ambalo ziara ya rais inafanyika.

Mbio za Atlas zinafanyika kwa mara ya pili mwaka huu ambapo gharama ya kujisajili kwa wakimbiaji wa kilometa 21 na kilometa 10 ni Sh. 30,000 wakati wale wa kilometa tano wakipaswa kujisajili kwa Sh. 25,000.

Washindi wa kwanza kwa kilometa 21 wataibuka na Sh. 400,000 kwa mwanaume na mwanamke wakati wa pili wakijizolea Sh. 250,000 watatu Sh. 200,000 na Sh. 150,000 kwa washindi wanne huku wa tano wakiondoka na Sh.100,000.

Mshindi wa kwanza kwa kilometa 10 ataibuka na Sh. 300,000, wa pili Sh. 200,000, wa tatu Sh. 150,000 huku wanne wakiondoka na Sh. 100,000 na wa tano Sh. 30,000 kwa jinsia zote.

Kwa wakimbiaji wa kilometa tano, washindi wa kwanza watajinyakulia Sh. 100,000, wa pili Sh. 75,000, wa tatu Sh. 50,000 na wanne Sh. 20,000 kwa jinsi zote mbili.

## TFF yajikita kuibua makocha wa kike

**Shufaa Lyimo na Adam Nyangasa, TUDARCo**

RAIS wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, amesema mkakati wao kwa sasa ni kuhakikisha Tanzania inakuwa na makocha wengi wa kike watakaozinoa timu za wanawake tofauti na ilivyo sasa ambapo kazi hiyo imekuwa ikifanywa na makocha wa kiume.

Karia alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kozi ya ukocha kwa upande wa wanawake ambayo itafanyika kwa muda wa siku tano, kwenye ofisi za makao makuu ya shirikisho hilo zilizopo Karume, Ilala.

Aidha, Karia aliwataka washiriki wote wafuate kwa makini mafunzo hayo na kwa kuwa lengo la TFF ni kuendelea kufanya hivyo kwenye mikoa mingine nchini.

"Mafunzo haya yana faida sana kwa wanawake, tunafahamu tutakuwa na walimu wenye weledi mkubwa wa kufundisha mpira wanawake," alisema.

Alisema ili mpira wa Tanzania uweze kukua wanawake hawana budi wajitokeze kwa wingi wanaposikia fursa hizo kwa kuwa mafunzo hayo wanayatoa bila malipo yoyote.

Karia alisema kupitia mafunzo hayo wanatarajia kupata wakufunzi wengi wazuri ambao watakwenda kuyatumia kwa manufaa yao na kwamba kwa baadaye hayatatolewa tena bure kama ilivyo kwa sasa.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Soka la Wanawake nchini, Amina Karuma, alisema ameyapokea mafunzo hayo kwa furaha kubwa na kudai yanalengo la kuhakikisha mpira wa wanawake unakua.

Alisema walitarajia kuwa na washiriki 35, lakini mpaka jana walikuwa 30 na kudai kozi hiyo ina faida kubwa kwa wanawake.

## Kamati ZFF yaanza kupitia usajili Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imeanza mchakato wa kupitisha fomu za usajili za wachezaji kuelekea kuanza msimu mpya wa 2020/21.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Mohammed Ameir, alisema wiki hii kamati hiyo inatarajia kupitisha fomu za usajili kwa timu za Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na Pemba pamoja za wachezaji wa Ligi Kuu Zanzibar.


Alisema kamati hiyo inataka kuharakisha zoezi hilo ili kutoa muda kwa klabu kuwasilisha pingamizi.

Alisema changamoto zilizopo katika kazi hiyo ni zile zile ambazo zimekuwa zikijitokeza kila msimu, hususan uliopita ikiwamo suala la baadhi ya wachezaji kushindwa kuandika majina yao kwa ufasaha.

Mkurugenzi huyo alisema majina yanayoleta utata ni yale ya Mohammed (Moh'd, Mohmed), na Abdalla, Abdallah, Abdala, pamoja na Ally, Ali, Alli, ambayo mara nyingi hayafanani na yaliyopo katika vyeti vyao vya kuzaliwa.

Mbali na changamoto hiyo ya majina, lakini klabu nyingi zimekuwa zikishindwa kujua ngazi husika za kufanya usajili.

Michezo
Jumanne Oktoba 13, 2020
Nipashe



## RAIS AKATAA MESSI NI MBELEKO YA LALIGA

HABARI UK 22

TUTA NYAVUNI...



Mshambuliaji wa England, Marcus Rashford, akiisawazishia timu yake kwa mkwaju wa penalti wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ubelgiji kwenye mechi ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya iliyopigwa katika Uwanja wa Wembley usiku wa kuamkia jana. **HABARI UK. 20.**

# NDAYIRAGIJE KUMTAFUTIA DAWA MSUVA, SAMATTA

Hesabu za mabao ya Taifa Stars ikiiwinda Tunisia azipata kwa Burundi baada ya kukiri...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu ya Taifa ya Burundi 'Intamba Murugamba', kumwonyesha udhaifu wa kucheka na nyavu unaoikabili Taifa Stars, Kocha Mkuu wa kikosi hicho cha Tanzania, Etienne Ndayiragije, amesema kazi inayomkabili kwa sasa ni kutafuta 'dawa' ya kumaliza tatizo hilo kwa safu yake ya ushambuliaji inayoongozwa na nahodha Mbwana Samatta akisaidiana na winga Simon Msuva.

Katika mechi hiyo ya kirafiki ya kimataifa iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na Burundi kushinda bao 1-0, shukrani zikimwendea Said Ntibazonkiza aliyeipa ushindi huo wakati zikiwa zimesalia dakika sita mechi kumalizika, Stars ilimiliki mpira kwa asilimia kubwa huku ikitengeneza nafasi na kufika langoni kwa wapinzani wao, lakini tatizo kubwa lilikuwa ni umaliziaji.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Ndayiragije alisema timu yake ilicheza vizuri, lakini tatizo kubwa lilikuwa ni kulazimisha kuingia kwenye eneo la hatari na kupiga mashuti golini.

"Kama uliona kipindi cha kwanza, tulifika golini kwa Burundi mara nyingi, lakini tulipiga shuti moja tu lililolenga lango, kwa hiyo inaonekana hatujawa makini kwenye umaliziaji," alisema Ndayiragije.

Alisema timu zote mbili, Tanzania na Burundi zilicheza vizuri, lakini kwa upande wa Taifa Stars sehemu zote ilicheza vema, ila tatizo lilikuwa kwenye kumalizia licha ya kupata nafasi nyingi.

"Nimeona wapi tumeishia, kwa sababu ukiona timu mpaka inatoka nyuma na kufika hadi mbele ujue kuna kitu kimefanyika, timu imetengenezwa, tatizo la umaliziaji nimeliona na nitalifanyia kazi. Kama tunafika golini na tatizo ni kumalizia, basi nina imani tutafanyia kazi hayo," alisema.

Katika mechi hiyo Stars pia ilikosa mabao ya wazi kupitia kwa Samatta, Said Ndemla, Shomari Kapombe, Idd Nado aliyekosa mara mbili, na Msuva.

Aidha, Ndayiragije alisema Stars imeanza kupata 'shape' (sura) anayohitaji mbeleni na sasa suala lililobaki ni kufanyia tu kazi safu ya ushambuliaji upande wa umaliziaji kabla ya kuikabili Tunisia.

"Tutafanyia kazi mapungufu haya machache, hasa katika umaliziaji wa nafasi tunazozitengeneza, tulikuwa na matatizo ya kulazimisha kufunga maeneo yasiyohitajika na haraka zisizo na umakini katika eneo la mwisho," alisema Ndayiragije.

Kwa upande wa Kocha wa Burundi, Jimmy Ndayizege, alisema timu zote zilicheza vizuri na wapinzani wao, Stars walibadilika kipindi cha pili kwa kupata nafasi nyingi za wazi na kushindwa kuzitumia.

Alisema wametumia mapungufu ya Tanzania na nafasi chache ikiwamo moja muhimu iliyowapa ushindi huo.

"Mechi ilikuwa nzuri timu zote zilipambana, kwetu ilikuwa ni mchezo wa kulipa kisasi, Tanzania walipata nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia na kwetu tumetumia nafasi hiyo," alisema Ndayizege.

Taifa Stars inajiandaa na mechi ya kufuzu kucheza fainali za AFCON dhidi ya Tunisia kwenye Kundi J, Novemba 13 ugenini na marudio yakiwa siku nne baadaye jijini Dar es Salaam.

Kwenye kundi hilo Tanzania inashika nafasi ya tatu ikiwa na alama tatu baada ya kucheza mechi mbili, ikishinda moja na kufungwa moja, huku vinara wakiwa ni Tunisia na Libya ikishika nafasi ya pili wakati Equitorial Guinea ikiburuza mkia.

## MORRISON, YANGA KIMEELEWEKA TFF

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI akitarajiwa kuwa miongoni mwa wachezaji watakaoshuka dimbani leo kuivaa Ndanda FC, Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), imesema malalamiko ya Yanga kuhusu dosari za mkataba wa Bernard Morrison na Simba, tayari yameiva baada ya kukutana jana.

Simba itashuka katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam leo kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Ndanda FC ambayo katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi Daraja la Kwanza, ililazimisha sare dhidi ya African Lyon kwenye Uwanja wa Uhuru.

**Hata hivyo, jana Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF, chini ya Mwenyekiti wake, Elias Mwanjala, ilikutana kupitia mambo mbalimbali ikiwamo malalamiko ya Yanga iliyoyatoa hivi karibuni kupitia kwa Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Frederick Mwakalebela, kuwa mkataba kati ya Simba na Morrison unadosari kwa kile alichodai kuwa hauna saini yoyote ya kiongozi wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao.**

Mwenyekiti huyo alimwambia mwandishi wetu jana kuwa, tayari wamepitia malalamiko hayo na leo kila kitu kitawekwa hadharani kuhusu hatima waliyofikia.

Hata hivyo, Yanga inacheza pande mbili katika sakata hilo, kwani mchezaji huyo aliishtaki klabu hiyo kwa kamati hiyo na kuibwaga chini katika kesi yake ya kudai kughushiwa kwa mkataba wake baada ya ule wa awali wa miezi sita kumalizika.

Lakini Yanga ilieleza kuwa imewasilisha rufani yao Mahakama ya Usuluhishi ya Masuala ya Michezo (CAS), ambapo kwa sasa inasubiri majibu hayo pamoja na haya ya leo kutoka kwa Kamati hiyo ya TFF.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002